MAISHA YA Sh. MUHAMMAD KASSIM AL-MAAMIRY

(1850 – 1910)

Ghalib Yusuf Tamim Baalawy

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni Mwanachuoni aliyekua Kadhi Mkubwa wa Mwambao wa Pwani ya Africa Mashariki kuanzia 1875 hadi 1910. Alisifika sana katika uamuzi wa Kesi ya Rufaa iloletwa kwake - Kadhi wa Zanzibar wakati huo akiwa ni Syd. Ahmad bin Sumayt.

DIBAJI YA MTUNGAJI

MAISHA YA Sh. MUHAMMAD KASSIM AL-MAAMIRY (1850-1910)

Alhamdu Lillah! Namshukuru Allah kwa kuniwezesha kuandika kitabu juu ya Mwanachuoni huyu aliyesifika sana wakati wa uhai wake kwa wekevu (*intelligence*), tabia bora, uhodari wa kusema na kuamua kesi zilizoletwa kwake, *A'lim* ambae hakuogopa kusema kweli na kuitetea haki. Kitabu hiki kinafuata kile cha Sh. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui (1825-1894) nilicho kitoa 2014. Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ndiye aliyekuwa Mwanafunzi Mkubwa wa Sh. Ali b. Abdalla. Akamfuata Shekhe wake hatua kwa hatua, mpaka akakubalika kuwa yeye ndiye Mfuasi halisi (*disciple*) wa Sh. Ali b. Abdalla - kielimu, tabia, mwenendo, ukakamavu, uhodari pamoja na ucha Mngu, Alhamdu Lillah! Insha'Allah Mwenye-ezi-Mngu awajazi kheri kwa kazi walizozifanya za kuzalisha vizazi vya Ma-Ulamaa walobobea. Insha'Allah malipo yao ni Jannatul Firdaus – Amin.

Kila Mtafiti (*Researcher*) wa Tareikh ya Wanavyuoni na viongozi wa kidini wa Afrika ya Mashariki, hautimii utafiti wao ikiwa hawajatumia kiegezo cha kitabu mashuhuri cha Sh. Abdalla Swaleh Farsy (1912-1982), aliyekuwa Kadhi wa Zanzibar. Baada ya mapinduzi ya Unguja 1964, na baada ya kustaafu kwa Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** (1912-1982) kama Kadhi Mkuu wa Kenya, Sh. Abdalla Farsy alishika Ukadhi Mkuu wa Kenya kwa miaka mingi. Sh. Abdalla na Sh. Muhammad Kassim Mazrui walikuwa marafiki wakubwa baada ya kujuana wakiwa wote wawili ni wanafunzi wa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947). Wakati alipopelekewa habari za kufa kwa Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** mwaka wa 1982, Sh. Abdalla Farsy baada ya kushukuru kwa kuondokewa na kipenzi chake, alisikika akisema, "Na mimi nimeshakufa!" Na kweli mwaka huo huo wa 1982 baada ya kama miezi sita, na yeye pia akaaga dunia na kuungana na swahibu yake katika barzakh.

Hapa ninamnukuu Sh. Abdalla Swaleh Farsy juu ya Sh. Muhammad Kasim **Al-Maamiry** katika kitabu hicho kinachotumiwa na wa-Tafiti, kiitwacho, ***"Baadhi ya Wanavyuoni wa KiShafi wa Mashariki ya Afrika"*** toleo la June 1972:

Katika mabwana wakubwa wa Mashariki ya Afrika waliosoma kwa Sh. Ali bin Abdalla – ima Unguja na Mombasa au Mombasa tu – ni hawa:

(a) *Sheikh Muhammad bin Kasim Al-Maamiry aliyezaliwa Mombasa mwaka 1266 A.H. (1850) akafa huko Mombasa siku ya Al-Khamisi mwezi 26 Mfunguo tatu mwaka 1372 A. H. (19 January 1910), naye ni mtu wa miaka 62. Huyu ndiye mwanafunzi mkubwa kabisa wa Sh. Ali bin Abdalla na ndiye aliyeshika mahali pake, akawasomesha wanafunzi wenzake wote baada ya kufa shekhe wao. Sheikh Suleyman bin Ali Al-Mazrui na Sh. Ahmad Mlomry ni miongoni mwa hao wanafunzi wenziwe waliosoma kwake sana. Akikamata kazi hii muda wa miaka 16 – tangu kufa shekhe wake mpaka kufa kwake. Bwana huyu hakuwa mwanachuoni tu mkubwa wa Mombasa bali alikuwa Kadhi wa hapo pia. Akashukuriwa katika hukumu zake na katika kufundisha kwake watu dini. Jina lake linadumu mpaka leo kwa mambo yake mazuri niliyoyataja na kwa ajili ya mwanawe – Sh. Muhammad bin Muhammad bin Kasim – ambaye ni mmoja mwa mawakili mashuhuri katika Kenya.*

Kwa kumnukuu Sh. Abdalla Swaleh Farsy juu ya kitabu chake hicho, na kwa urafiki ulokuwepo baina yake na Sh. Muhammad Kassim **Mazrui**; na kwa bahati niloipata mimi kwa Mashekhe na Maulamaa hao wawili, nachukua fursa hii ya kukipendekeza kitabu hiki kuwa ni kumbukumbu zangu kukiegeza kwao.

Bahati niloipata mimi ni kulelewa na Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** miaka sita ya mwanzo katika utoto wangu. Na ukubwani mwangu nimebahatika kwa miaka mingi kuwepo katika vikao vyao vya kupokea na kuyakinisha kwa kuandama na kumalizika kwa mwezi wa Ramadhani. Vikao bora kabisa ni vikao vya Maulamaa. Kuwepo kwangu si kwa kuwa ni Msomi, bali ni bahati ya kuwa ni mmoja kati ya wa watu wa nyumbani kwa Sh. Muhammad Kassim Mazrui. Namshukuru Allah kwa kunipa bahati hiyo – Alhamdu Lillah!

Jukumu la kuandika na kumzungumza Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, chanzo chake ni Ustadh Athman Naaman, Imamu wa Msikiti

wa Mazrui. Ustaadh Naaman ameanzisha Muhadhara wa kuwazungumzia Wanavyuoni wetu wakati wa likizo la December. Mwaka wa 2011, Sh. Hammad Muhammad Kassim Mazrui alimzungumza Sh. Suleiman b. Ali b. Khamis Mazrui. December 2012 nikapewa jukumu la kumzungumza Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui. 2013 nikamzungumza Sh. Ali b. Abdalla b. Naf'i Mazrui na 2014 Alhamdu Lillah nikamzungumza **Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry**.

Alhamdu Lillah! Bw. Muhammad Basawad na Ustadh Naaman wamefanya mipango kamili na kutoa DVD ya hotuba hizo, zinazo patikana katika Maktaba yao ya "The Qur'an and Sunna Association of East Africa" iliopo Taj Mahal, Mombasa. Vile vile namshukuru Allah kwa kuniwezesha kuchapisha vitabu vya Wanvyuoni hao watatu - 2006 juu ya Sh. Al-Amin, na mwanzo wa 2014 juu ya Sh. Ali b. Abdalla na Insha'Allah hiki cha Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry mwisho wa 2015.

هذا من فضل ربى – الحمد لله!

Nataka kutowa shukrani zangu za dhati kwa:

1. Mzee Rashid Abdalla Mazrui (1934-2015) wa Takaungu (jina maarufu – Babu!). Nilipata kutoka kwake hoja za kwanza juu ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry wakati nilipomuhoji juu ya ***"Lulu ya Takaungu – Maisha ya Ramla Rashid Abdalla Mazrui."*** Baada ya kutambua kuwa Mzee Rashid ana kumbukumbu nyingi juu ya wanavyuoni wetu alizozipokea kutoka kwa babaake, nimefunga safari mara nyingi kumuhoji juu ya Maulamaa mbali mbali, akiwemo Sh. Ali b. Abdalla na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry. Mzee Rashid alifariki 22 July 2015. Allah amlaze pema na amlipe Jannatul Firdaus kwa wema wake mkubwa.
2. Maalim Abdurahman Saggaf wa Mombasa, mzaliwa wa Wasini. Huyu, Masha'Allah! Ana kumbukumbu nyingi sana juu ya Tareikh ya Wanvyuoni na wakazi wa Pwani kwa ujumla. Nimemuhoji mara nyingi juu vitabu vyangu vyote vitatu.
3. Ustadh Harith Swaleh wa Lamu, mkazi wa Mombasa. Masha'Allah! Ustadh Harith ni ***'Alim***, alobobea katika Tareikh za wanavyuoni wetu. Nimebahatika kumuhoji juu ya kitabu hiki.

4. Ndugu yangu kipenzi, Bw. Salim Ahmad Muhsin Maamiry, kitukuu cha Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry. Juu ya kuwa Salim tumekulia na kucheza pamoja, sikuwa nikijua kuwa Masha'Allah amepokea mengi sana juu ya baba wa babu yake. Nilielekezwa kwa Salim na Ustadh Harith. Alhamdu Lillah! Nilimuhoji Salim kwa masaa mengi, nikadondoa mengi ambayo nisingeyajua namna ya kuyapata, hasa yale ya kinyumbani. Ikawa mahojiano yetu ni kuurudisha upya udugu wetu. Mimi nikiwa kitukuu cha Ali b. Abdalla na yeye ni kitukuu Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry. Wanavyuoni hao wawili wakiwa ni mtu na mwanafunzi wake – Subhana Allah!
5. Swahibu yangu, Imamu wetu wa Msikiti wa Mazrui, Ustadh Athman Naaman kwa kuanzisha Mihadhara na kuhuisha Tareikh ya Maulamaa wetu. Yeye ndie aliyenitweka jukumu la kuwazungumza Wanavyuoni hao watatu katika Mihadhara yake ya December katika Msikiti wa Mazrui.
6. Ndugu kipenzi na Mwendani wangu katika misururu ya vitabu vyangu, Al-Akh Muhammad bin Yusuf (Ibn Yusuf), mkazi wa Toronto, Canada. Yeye ndiye Mshauri na Mhariri wa vitabu vyangu vyote.

Napenda kuwashukuru kwa dhati hao nilowataja hapo juu, na kila ambae alichangia kwa njia moja au nyengine juu ya kufanikiwa kukichapisha kitabu hiki. Nawaombea, "Allah awajazi kila la kheri duniani na Akhera – Amin."

Likiwepo kosa lolote katika kuhadithia maisha ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, kosa hilo ni langu na naomba msamaha kuanzia mwanzo, kwani Ukamilifu ni wa Allah. Na ikiwa nimesibu basi nawatakia na hao nilopokea kutoka kwao ujira wa kazi hii pevu.

Wa Billahi Tawfiq.

غالب يوسف تميم باعلوى

Ghalib Yusuf Tamim Baalawy

gytamim@yahoo.com
+254721631178

24th August, 2015

UTANGULIZI WA MAISHA YA SHEIKH MUHAMMAD KASSIM AL-MAAMIRY

Ghalib Yusuf Tamim ameongeza kitabu cha tatu katika mfululizo wa vitabu vyake vya Maulamaa wetu wa Mombasa. Vitabu hivi ni vitabu muhimu sana kwa sababu nyingi.

Sababu moja kubwa ni kuwawezesha Wataalamu wetu wa leo kufahamu mabega ambayo yaliyo wainuwa wao kufika pale ambapo wameweza kufika. Ilmu huzaa ilmu na fikra huzaa fikra. Na fikra zinazo tuathiri leo zatokana na mtilizi wa fikra ambazo zatoka mbali. Yasemekana kuwa katika zile zama za Spain ilipokuwa katika mikono ya Waislamu, kulikuwa na Chuo Kikubwa cha Cordoba. Chuo hicho kilikuwa maarufu sana na wanafunzi waliokuwa wakisoma hapo walikuwa wengi ni Waislamu, lakini si wote. Baadhi yao walikuwa ni Mayahudi na baadhi yao walikuwa ni Wakristo. Hawa hawakwenda hicho Chuo cha Kiislamu kusoma Uislamu au kusoma Uyahudi au kusoma Ukristo. Walikwenda kusoma jinsi Wataalamu wa Kiislamu wanavyo bahith ule Uislamu ili na wao wapate kutumia silaha hizo hizo katika kubahith dini zao. Cordoba ilikuwa ni kiini cha chemchemu ya ilmu ya Uislamu. Yasemekana kuwa fikra ambayo iliyotolewa Cordoba ilitambaa katika mikondo ya Vyuo vya Timbuktu, Fez, Al Azhar, Makka, Madina mpaka kufika Basra katika Iraq. Kila ipitapo fikra ile iliongezwa sherehe na iliporudi Cordoba ilikuwa ni kitabu kizima! Hivi ndivyo ilmu ya Uislamu ilivyokuwa yaenea baina ya Wataalamu mbali mbali. Hivyo ilikuwa ndio mwanzo wa kile tunachoita leo kwa jina la *International Journal*.

Ukitaka kuujuwa Ummah wa Kiislamu wa nchi kadha, basi watafute Wataallamu wa pahali hapo. Ummah usiokuwa na Wataallam ni Ummah ambao ushakufa au uko njiani kwenda kwenye kifo. Sheikh Ghalib Tamim ametufanyia sote ihsani kwa kutuwezesha kuinua nyuso zetu kwa kutukumbusha sisi na wengineo kuwa nasi pia tutiwe katika hisabu ya watu kwani watu ni ilmu yao. Na ilmu ya watu ni Wanazuoni wao. Basi yatupasa kumshukuru sana Ghalib kwa bidii aliyoifanya mpaka hivi kuyadhibiti maisha ya hawa Wataallam watatu: Sheikh Ali bin Abdalla, Sheikh Al-Amin bin Ali na sasa Sheikh Muhammad Kassim Al-Maamiry.

Lakini pia twataka kukumbuka kuwa Ummah wetu si Ummah wa Mombasa pekee. Ummah wetu waenea kutoka Mogadisho katika Somalia mpaka Ngazija na kupendukia. Na kote huku kulikuwa na Wataalamu ambao walikuwa wakieneza Dini ya Uislamu na fikra mpya mpya za Dini yetu. Hii ni kusema kuwa Sheikh Ghalib atukumbusha kuwa kazi hii ya kuyatafiti na kuyanakili maisha ya Wataallam wetu ni kazi ambayo sote twahitajiwa kuifuata kwa hima – filhali na filmali. Katika kumshukuru Sheikh Ghalib twataka pia kumuomba aendelee na kazi aliyoianza ili na wengine waingiwe na hamu ya kuiendeleza kazi hii. Kwa upande mmoja kuna wazee ambao bado walikuwa wakiwajua hao Wataallam kwani kila uchao na wao warudi kwa Mola wao.

Lakini kazi hii aifanyayo Sheikh Ghalib haifai kusimama kwa Wataalam wa Dini peke yake. Wataallam wa Dini walikuwa wakisomesha kwa lugha ya Kiswahili. Na yoyote ambaye amejaaliwa kusikiza darsa zao alikuwa ajuwa akipata raha ya kujuwa dini na kujuwa lugha ya Kiswahili. Ilikuwa ni raha kusikiza tafsiri ya Quran na ya vitabu vyengine vya dini kwa lugha ya Kiswahili swafi ambacho hakina tone ya lugha ya Kiengereza. Na maandishi yao pia yalikuwa ni maandishi ya lugha swafi ya Kiswahili. Ni bahati mbaya kuwa tafsiri za darsa za Wataalamu hawa hazikupata kunakiliwa kwa mitambo ya kushika maneno. Lakini wakati wa Wataallam kama kina Sheikh Abdalla Saleh Farsy, mitambo hayo yalikuwako. Na katika 1950s, watu kama AlMarhum Sheikh Hyder Muhammad Matano aliwanakili watu wengi katika ufuo wa Pwani katika kipindi chake cha Radio kilichokuwa kikiitwa MVITA NA PWANI YAKE.

Ni muhimu sana kuwa wale wanao fuata mfano mzuri wa Sheikh Ghalib kutumia na vifaa vyovote vitakavyo patikana ili kubahith maisha ya watu wetu – Wataallam na wasiokuwa Wataallam -- kwani wote ni wenye kumulika muangaza juu ya maisha yetu. Ikiwa vijana vyetu vya leo na vya kesho wapawe nafasi ya kujijuwa usuli wao na utu wao, itatakikana kupawa nafasi ya kusoma vitabu hivyo. Ni niya yetu hapa MUSLIM CIVIC EDUCATION TRUST (MCET) kuchochea muendelezo huu kwa hali na mali. Sababu yake ni kuwa ikiwa Ummah wa Kenya wataka kuendelea na kujinaki na utamaduni ambao watazidi kuleta Kenya, ni muhimu mwanzo kujuwa watoka wapi.

Wa Billahi Tawfiq

PROFESSOR MUHAMMAD HYDER

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry (1850-1910)

Jee Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni nani?

- Sh. Muhammad bin Kassim Al-Maamiry alizaliwa mji wa Mombasa mwaka wa 1850 na kufariki Mombasa, Al-Khamisi 19 January 1910.
- Yeye ndiye aliyekuwa Mwanafunzi Mkubwa wa Sh. Ali b. Abdalla b. Naf'i Mazrui (1825-1894).
- Alipokufa Sh. Ali b. Abdalla mwaka wa 1894, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa na umri wa miaka 44. Jukumu la kuziendeleza Darsa za Shekhe wake likamuangukia yeye. Alhamdulillah akaziendeleza Darasa hizo mpaka kufa kwake kwa muda wa miaka 16.
- Alihitimu kuishikilia nafasi hiyo kwa kupata Ijaza kutoka Sh. Ali b. Abdalla na akawa Mwalimu wa wanafunzi wenzake akiwemo Sh. Suleiman b. Ali b. Khamis Mazrui (1867–1937, wakati huo akiwa na umri wa miaka 27). Sh. Suleiman ni Mlezi, Mwalimu na Mkwe wa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947). Mwanafunzi mwenza, nae aliyerudi kuwa mwanafunzi wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni Sh. Ahmad b. Muhammad Mlomry (1873-1936, nae wakati huo akiwa na umri wa miaka 21). Sh. Mlomry ndiye aliyekua Mwalimu wa Sh. Abdalla Swaleh Farsy (1912-1982).
- Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kwa kutambulika kuwa ni *A'lim*, alichaguliwa kuwa Kadhi wa Mombasa (kutoka 1875 hadi kufa kwake 1910). Alishika Ukadhi baada ya Sh. Rashid b. Abdalla Naf'i (aliyekuwa Kadhi kutoka 1870 hadi 1875). Huyu ni nduguye Sh. Ali b. Abdalla Naf'i (Sh. Ali alikuwa Kadhi 1856 hadi 1870). Sh. Rashid nae pia aliwahi kusoma kwa kakaake.
- Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa Kadhi shupavu, aliyeweza kuamua na kutoa hukmu zenye kukubalika. Ikawa mpaka analetewa kesi za Rufaa kutoka Zanzibar kama tutakavyo elezea baadae – Insha'Allah!

TANZU MBILI

سُبْحَٰنَ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلْأَزْوَٰجَ كُلَّهَا مِمَّا تُنۢبِتُ ٱلْأَرْضُ وَمِنْ أَنفُسِهِمْ
وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾

Surah Yasin 36:36 *Subhana, Ametakasika yule ambaye ameumba jeuzi mbili mbili katika kila alichokiumba, katika vinavyo mea katika ardhi na katika nafsi zao, na* ***katika wasivyo vijua****.*

Naanza kukiandika kitabu hiki kwa **Kalima Mbili**:

- Bismi Llahi, na
- Alhamdu Lillahi!

Tena kwa **Sifa mbili** za Allah:

- Ar-Rahman – Mwingi wa Rehema
- Ar-Rahim – Mwenye Kurehemu.

Watu wawili walinijaza mahaba ya kumpenda mpaka kunipelekea kuandika juu ya *Maisha ya Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947)*:

- Mamaangu, Bi Aisha binti Al-Amin Mazrui (1927-1988)
- Mwalimu wangu, Maalim Twalib Swaleh Elyan (1939-2015)

Watu wawili walinipa changamoto mpaka wakanipelekea kuandika juu ya *Maisha ya Sh. Ali b. Abdalla Naf'i (1825-1894)*:

- Ustadh Athman Naaman, Imam wa Msikiti wa Mazrui
- Kadara Harith Swaleh, mwanawe Ustadh Harith Swaleh

Athari mbili kwa **njia mbili** tafauti alizoziwacha Sh. Ali b. Abdalla Naf'i:

- Urathi kwa njia ya chembe-chembe za uzazi (*Genetically – DNA*) – Mwana *Alim*, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui

- Urathi kwa njia ya kusomesha upeo wa elimu na juhudi na kumtayarisha kuwa kama kivuli chake (Swahaba - *Disciple*) – Mwanafunzi *Alim*, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.

Baada ya kuandika juu ya Maisha ya **Ma-Ulamaa wawili**:

- Juu ya Mwana, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui
- Na juu ya Baba, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i,

Ilikuwa hapana budi ila kujitahidi na kufanya utafiti wa kuyaandika maisha:

- Juu ya Mwanfunzi, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.

Watu wawili walichangia sana wakati wa kuandika juu ya *Maisha ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry (1850-1910)*:

- Ustadh Harith Swaleh, babaake Kadara
- Mzee Rashid Abdalla Mazrui (1934-2015)

La ajabu zaidi ni kuwa kitabu hiki ni mchango wa **vitukuu wawili**:

- Ghalib Yusuf Tamim – Kitukuu wa Mwalimu, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i
- Salim Ahmad Muhsin – Kitukuu wa Mwanafunzi, Sh. Muhammad Kassim al-Maamiry.

Wapili katika Wawili

Sayyidna Abubakar As-Siddiq (A.S.) alipata sifa ya kua Mwendani wa Mtume Muhammad (S. A.W.) – yeye ndiye aliyekua Swahiba wa Karibu na Khalifa wa Kwanza wa Mtume (S. A. W.). Yeye ndiye aliekua kama kivuli cha Mtume na ndiye Swahaba aliyefanana na Mtume kwa kila hali. Sayyidna Abubakar ndiye *Thaniya Thnaini* – Wapili katika Wawili, kama Chanda na Pete.

Tukitumia kiegezo hiki cha Mtume (S. A. W.) na Sayyidna Abubakar, huu ndio mfano bora baina ya Sh. Ali b. Abdalla Naf'i na Sh. Muhammad Kassim Al-

Maamiry. Tuwatizame watu wawili hawa katika darubini hiyo ya Wendani hao wawili.

- Sh. Ali b. Abdalla alizaliwa 1825, nae Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akazaliwa 1850.
- Sh. Ali alianza kusoma kwa babaake, Sh. Abdalla b. Naf'i Mazrui. Vile vile Sh. Muhammad alianza pia kusoma kwa babaake, Sh. Kassim Said Al-Maamiry.
- Sh. Ali pamoja na Mwanafunzi wake, Sh. Muhammad walizaliwa na kukulia katika Madhehebu ya Ibadhi.
- Sh. Ali akabadili Madhehebu yake ya Ibadhi na kufuata Madhehebu ya Shekhe wake, Sh. Ali b. Muhammad Surury Al-Misri.
- Nae Sh. Muhammad akabadili Madhehebu yake ya Ibadhi na kufuata Madhehebu ya Shekhe wake, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i.
- Alipokufa Mtume (S. A. W.), Sayyidna Abubakar (A.S.) ndiye aliyeshika nafasi yake, akawa ndiye Khalifa wa kuendeleza kazi za Mtume. Vile vile alipokufa Sh. Ali b. Abdalla 1894, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry aliziendeleza kazi za Shekhe wake mpaka kufa kwake 1910, kama alivyo tufundisha Mtume (S. A. W.).
- Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akajipamba na sifa njema za Shekhe wake, Sh. Ali b. Abdalla.

Allah anatueleza katika Qur'an:

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا۟ ٱللَّهَ
وَٱلْيَوْمَ ٱلْـَٔاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

Surah Al-Ahzab 33:21 *Bila ya shaka muna kiigizo kizuri kilo chema kutokana na Mtume wa Mwenye-ezi-Mngu kwa wale wenye kumuogopa Mwenye-ezi-Mngu na Siku ya Mwisho, na wakamtaja Mwenye-ezi-Mngu sana.*

Mwaka wa 1837 Sh. Ali b. Abdalla akiwa na umri wa miaka 12 alisafiri pamoja na babaake na nduguye – Sh. Abdalla Naf'i na Sh. Ahmad Abdalla Naf'i, wakaondoka kwao Mombasa na kuhamia Makka kwa masomo. Kabla hawajaondoka, Sh. Ali alimuandikia babaake Msahafu ili watakapofika Makka, baba autumie kwa masomo yake ya Elimu ya Tafsiri ya Qur'an. Msahafu ambao baba alikua akiuandika pambizoni mwake kile anachokipata kutoka kwa Shekhe wake, Sh. Ahmad b. Muhammad Ad-Dimyaty.

Baada ya miaka tisa, wote watatu wakijiendeleza kimasomo, baba na mwana mmoja, Sh. Ali b. Abdalla wakafunga safari ya kurudi kwao, Mombasa. Sh. Ahmad b. Abdalla akaamua kubaki na kufanya makazi yake huko huko Makka. Walipofika Bandari Shihr kabla ya kupanda marekebu na kuanza safari, baba-mtu akaugua na kufa. Baada ya mazishi, Sh. Ali b. Abdalla akiwa tayari ni Msomi mwenye umri wa miaka 21 akarudi kwao Mombasa, mwaka wa 1846. Waliondoka wakiwa wote ni Ibadhi na wanarudi wakiwa wamebadili Madhehebu na kuwa Sunni. Sh. Ali anarudi kwao Mombasa kuanza kazi ya kusomesha. Na katika kusomesha kwake, ikawa anawavutia wanafunzi wake katika Usunni. Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akawa ni mmoja kati ya wanafunzi walotoka katika U-Ibadhi na kuvutiwa katika U-sunni.

Kwa kiu kubwa alokuwa nayo ya elimu, mwaka wa 1854 akarudi tena Makka na pia kwenda Hadhramout kujiendeleza kimasomo hadi 1856. Kwa mara ya tatu na ya mwisho 1858-1859 akarudi tena Makka na kuendelea na masomo. Labda safari hizi tatu za kimasomo, kwa lugha ya kileo tunaweza kusema kuwa alikwenda kwa Shahada ya *Bachelors*, *Masters* na baadae *PhD*.

Baina ya 1856 na 1870, Sh. Ali b. Abdalla alihudumu kama Kadhi wa Mombasa. Huu ulikuwa ni wakati wa Ufalme wa Sayyid Majid b. Said.

Mahusiano ya Sh. Ali b. Abdalla na wafalme wa Unguja yalichukua mkondo ufuatao:

- Sayyid Majid b. Said (Ufalme, 1856-1870) – alimuheshimu Sh. Ali b. Abdalla na kumchagua kuwa Kadhi wa Mombasa kwa muda huo wa ufalme wake.

- Kadhi Mkubwa wa Ki-Ibadhi huko Unguja, Sh. Muhammad b. Ali b. Muhammad al-Mendhry aliandika kitabu alichokiita, *Khulaastud Daamigha* kuushambulia Usunni.
- Sayyid Majid kwa kujua kuwa Sh. Ali b. Abdalla alikuwa ni Sunni aliyeuhama U-Ibadhi, alimuuliza kama ameshakiona kitabu cha Sh. Muhammad Al-Mendhry.
- Sh. Ali b. Abdalla akajibu kuwa amekiona. Akaulizwa kama anaweza kuandika na kukijibu kitabu hicho. Jawabu ya Sh. Ali ikawa "Lau kama si kustahi Madhehebu yako ningekijibu".
- Sayyid Majid akampa ruhusa Sh. Ali b. Abdalla kukijibu. Kwa hivyo Sh. Ali akaandika kitabu, *Adduruu Saabigha*, na kumuomba Sayyid Majid awaalike Ma-Shekhe wa Ki-Ibadhi na Ki-Sunni ili amjibu Sh. Muhammad Al-Mendhry katika muhadhara huo. Jawabu ya Sh. Ali b. Abdalla iliwaumiza sana Ma-Ibadhi, ikumbukwe kuwa wakati huo Ma-Ibadhi ndio walokuwa juu, kwa kuwa ndiyo Madhehebu ya Wafalme.
- Sifa hizi za kujadiliana ndizo baadhi ya sifa walizozirithi mwana na mjukuu, Sh. Al-Amin Mazrui (1891-1947) na Prof Ali Mazrui (1933-2014).

- Sayyid Barghash b. Said (Ufalme, 1870-1888) hakuwa na urafiki na Sh. Ali b. Abdalla. Ya yumkini kuwa katika watu walioumizwa na jawabu ya Sh. Ali b. Abdalla kwa kitabu hicho, *Adduruu Saabigha*, ni Syd. Barghash. Inaonekana kuwa ndipo ilipoanza chuki ya Syd. Barghash kwa Sh. Ali b. Abdalla.
    - Mwaka wa 1887, Sh. Ali b. Abdalla alikwenda Pemba kuwatembelea jamaa zake wa Ki-Mazrui walioko huko.
    - Sh. Ali b. Abdalla kama kawaida yake akaweka darsa kusomesha. Baadhi ya jamaa zake wakaacha U-Ibadhi na kufuata U-Sunni.
    - Syd. Barghash alipopata habari hizo za raia wake kuuhama U-Ibadhi hakuweza kuvumilia tena. Mara moja akatuma marekebu kutoka Unguja na kwenda Pemba kumkamata Sh. Ali b. Abdalla.

- — Sh. Ali alipofika Unguja, Syd. Barghash akamwambia ”Nitakufunga mpaka ufe wewe huko kifungoni ama nife mimi.” Jawabu ya Sh. Ali ikawa, “Basi si mbali!”
- — Na kweli baada ya miezi kadha, March 1888, Syd. Barghash akafa na Sh. Ali akafunguliwa.

- Sayyid Khalifa b. Said (Ufalme, 1888-1925) alimuheshimu sana Sh. Ali b. Abdalla na kujenga urafiki mkubwa na yeye:
  - — Syd. Khalifa kabla ya kuchukua madaraka ya Ufalme alitaka aapishswe na Sh. Ali b. Abdalla. Kwa hivyo akatoa amri Sh. Ali afunguliwe.
  - — Sh. Ali b. Abdalla akafuliza kutoka gerezani moja kwa moja mpaka katika Kasri la Mfalme na kumuapisha Syd. Khalifa kiapo cha Ufalme.
  - — Jemedari wa Mazrui katika Ukanda wa Pwani ya Kenya, Sh. Mbaruk b. Rashid Salim Mazrui (aliyekuwa *Liwali wa Gasi* 1869-1896) alikuwa akiuhangaisha sana Ufalme wa Zanzibar.
  - — Syd. Khalifa alipendelea kuumaliza uhasama ulokuwepo baina ya Ufalme wa Ki-Mazrui wa Ukanda ya Pwani na wa Al-Busaidy wa Zanzibar.
  - — Syd. Khalifa akatafuta mtu ambae aweza kumpatanisha yeye na Sh. Mbaruk. Alipoelezwa kuwa swahibu yake, Sh. Ali b. Abdalla ni jamaa yake Sh. Mbaruk, na ndiye mtu pekee anae mweza Sh. Mbaruk, hapo alimuomba Sh. Ali amfanyie mpango wa kuwapatanisha.
  - — Sh. Ali b. Abdalla alipo hakikishiwa na Syd. Khalifa kuwa atakapoweza kumshawishi Sh. Mbaruk na kumleta Unguja, basi Sh. Mbaruk atapewa heshima yake na hatodhuriwa.
  - — Sh. Ali akapewa moja katika marekebu za Mfalme, akenda Gasi na akaweza kumshawishi Sh. Mbaruk na kuja nae Unguja.
  - — Sh. Ali b. Abdalla akafaulu kuwapatanisha Syd. Khalifa na Sh. Mbaruk. Ukaondoka utesi baina ya Wakuu hawa wawili.

Jee kuna mafungamano gani baina ya matokeo haya ya kimaisha ya Sh. Ali b. Abdalla na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry:

1. Sh. Ali b. Abdalla amesafiri bara na bahari akikusanya elimu na maarifa mbali mbali:
   - **1825-1836** - Mombasa, alikozaliwa na kuanza kusoma kwa babaake, Sh. Abdalla b. Naf'i
   - **1836-1846** - Makka, akasoma kwa Sh. Ali b. Muhammad Sururi Al-Misry kwa miaka saba na baadae akaungana na babaake kusoma kwa Sh. Uthman b. Hassan Ad-Dimyaty na kwa Sh. Ahmad b. Muhammad Ad-Dimyaty (Mufti wa Makka).
   - **1847-1854** - Mombasa - akisomesha
   - **1854-1856** Makka na Hadhramout - akijiendeleza kimasomo kwa Mashekhe wengi na kumalizia kwa Sh.Abubakar Matraf huko Mkelle.
   - **1856-1858** - Mombasa na Unguja – akisomesha
   - **1858-1859** Makka – akasomea zaidi Elimu za Hadith kwa Sh. Muhammad An-Nabrawy; na kusomea *Mantik* (*Logics*) kwa Sh. Nur Suleyman.
   - **[1856-1870]** - amehudumu kama Kadhi wa Mombasa.
   - **1860-1894** – akisafiri mara kwa mara katika Ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki kusomesha na kutembelea jamaa, akijenga mahusiano mapya katika safari zake hizi.

Kusafiri peke yake ni elimu ya kutosha, jee ikiwa safari hizo ni za kwenda kusoma, utakuwa *Alim* wa kiasi gani? Hivi ndivyo Mwenye-ezi-Mngu anavyo tusifia faida za safari:

أَفَلَمْ يَسِيرُوا۟ فِى ٱلْأَرْضِ فَتَكُونَ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَآ أَوْ ءَاذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا ۖ فَإِنَّهَا لَا
تَعْمَى ٱلْأَبْصَـٰرُ وَلَـٰكِن تَعْمَى ٱلْقُلُوبُ ٱلَّتِى فِى ٱلصُّدُورِ ﴿٤٦﴾

Suratul Hajj 22:46 *Jee! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, na masikio ya kusikia? Kwani*

> *hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.*

Kwa hivyo Sh. Ali b. Abdalla alikusanya lulu na marjani. Alhamdu Lillah amesomesha wengi, akazalisha Ma-Ulamaa wengi. Lakini kila mtafuta mali na elimu anatarajia wakati atakapoondoka ulimwenguni, atakuwa na mrathi (*successor*) atakae endeleza biashara na elimu alizo chuma na kuzikuza. Na ikiwa wataka Mrathi mzuri, basi ni lazima, umkuze, umsomeshe na umtayarishe vilivyo, ndipo atakapoweza kuziendeleza kazi zako. Na naam! Sh. Muhammad alikuwa mwanafunzi mwema aloivishwa akaiva.

2. Sh. Ali b. Abdalla kama tulivyotangulia kusema alizaliwa na kukulia kama Ibadhi. Kwa kusoma kwa *Ma-Ulamaa* mbali mbali ndiko kulipo mpelekea kutoka katika U-Ibadhi na kuwa Sunni baada ya kukinaishwa tofauti zilizopo baina ya Madhehebu hayo mawili. Kwa hivyo ilikuwa ni wajibu wake na yeye kuwakinaisha wanafunzi wake:
   - Wale walozaliwa kama Sunni awasomeshe zaidi na awakuze wazidi kuufahamu U-Sunni na kuongezea zaidi maarifa yao.
   - Na wale walozaliwa na kukuzwa kama Ibadhi ilimuwajibikia kuwakinaisha uhaba uliopo ili watapovuka wafahamu ni kwa nini wanatoka katika Madhehebu ya Ibadhi na kuingia Madhehebu ya Sunni. Kisha awazidishie ufahamu wao na kuzidi kuzipanda daraja za elimu na kufahamu undani wa Madhehebu yote.

Mwanafunzi anapo ipokea elimu ya Mwalimu wake kwa hali nzuri, mwanafunzi huyo huwa kindelezo cha Mwalimu wake.

Na hivi ndivyo alivyokuwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, kwani alikuwa mwanafunzi mwema aliyeweza kuziendeleza kazi za Mwalimu wake. Kwa kujazwa pupa na kiu za elimu na Shekhe wake, Sh. Ali b. Abdalla, Sh. Muhammad Kassim aliweza kuwakia na kuwazidi wanafunzi wenzake kwa daraja kubwa. Ikatimia azma ya Sh. Ali b. Abdalla Naf'i ya kupata Mwendani wake, Mrathi wake na *Thaniya Thnaini* wake!

Sh. Ali b. Abdalla ikawa amepata kasha (*receptacle*) la kuweza kuhifadhi chumo lake la elimu, tabia, mwenendo na Mrithi (*disciple*) kamili. Akaweza

kumjaza Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry mahaba ya dini na taqwa, akampamba kwa tabia njema za kila aina. Na kwa udugu na urafiki waliokuwa nao baina yao, wakaweza kuwa *Thania Thnaini*.

Mmoja katika Mashekhe wa Sh. Ali b. Abdalla huko Makka alitabiri kuwa Sh. Ali atazaa mwana atakaekuwa *Alim,* lakini atazaliwa katika jaa. Utabiri huu ulitimia mwisho wa maisha yake, na kumzaa, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui. Wakati alipokufa Sh. Ali b. Abdalla 1894, mwana huyu ana umri wa miaka mine tu! Mwana huyu akamkabidhi binamu wake, Sh. Suleiman b. Ali Khamis Mazrui.

Sh. Al-Amin akarithi elimu za babaake kupitia kwa Sh. Suleiman kwa njia mbili:

- Moja kwa moja kutoka kwa Sh. Suleiman kama Mlezi, Mwalimu na Shekhe wake.
- Kupitia kwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kwani ndiye aliyekuwa Mwanafunzi-mwenza na baada ya kufa Sh. Ali b. Abdalla akawa Mwalimu/Shekhe wa Sh. Suleiman.

KIZAZI CHA Sh. MUHAMMAD KASSIM AL-MAAMIRY



Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry aliowa wake wawili:

1. Bi Aweina Salim Bassamy aliyemzalia watoto watatu. Mtoto wa mwisho Bw. Muhsin Muhammad Kassim ndie alie kiendeleza kizazi cha babaake kama itakavyo fuata.
2. Bi. Khadija binti Juma Shikelly ndiye mke wa pili. Ingawa amemkalia Eda alipokufa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, walakin hakuzaa nae. Huyu ndiye mlezi wake Bw. Kibwana Shikelly, babaake Bw. Soud Shikelly, babu yake Dr. Khadija Shikelly.

Wajukuu na vitukuu vya Sh. Muhammad Kassim

Kama tulivyosema hapo juu, kizazi cha Sh. Al-Maamiry kiliendelezwa na mwanawe wa tatu, Bw. Muhsin Muhammad Kassim Al-Maamiry kama ifuatavyo:

I. Bw. Ahmad Muhsin M. K. Al-Maamiry

1. Muhsin 2. Salim 3. Muhammad 4. Aweina
5. Salma 6. Amria 7. Nura

II. Sh. Alamin Muhsin M. K. Al-Maamiry

1. Muhammad 2. Ahmad 3. Rashid 4. Majid
5. Amur 6. Asmaa 7. Fatma 8. Joha 9. Swabiha 10. Johaina
11. Busra 12. Hamud 13. Hadie 14. Shuweina

III. Sh. Abdalla Muhsin M. K. Al-Maamiry

1. Said 2. Ali 3. Muhsin 4. Amria 5. Shuweikha 6. Khadija
7. Nuru 8. Nadh'ha 9. Shamun

IV. Bw. Ghazal Muhsin M. K. Al-Maamiry

1. Abdalla 2. Sumri 3. Ali 4. Issa 5. Jamal

Mahusiano Ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry na Wenzake

	Jina	Kuzaliwa	Kufa	Mukhtasar
1.	Sh. Ali b. Abdalla b. Naf'i	1825	1894	- Mwalimu wa Sh. M.K. Al-Maamiry na Sh. Suleiman A. K. Mazrui na Sh. A. M. Mlomry - Kadhi/ Mombasa
2.	Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry**	1850	1910	- Anarithi Darsa za Sh. Ali b. Abdalla Naf'i na kuendelea kuwasomesha Sh. Suleiman A. K. Mazrui na Sh. A. M. Mlomry - Kadhi/ Mombasa
3.	Sh. Suleiman Ali Khamis Mazrui	1867	1937	- Mwalimu na Mkwe wa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui - Kadhi Mkuu/Kenya (1932-1937)
4.	Sh. Ahmad Muhammad Mlomry	1873	1936	- Mwalimu wa Sh. Abdalla Swaleh Farsy
5.	Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui	1891	1947	- Mwalimu wa Sh. Muhammad K. **Mazrui** na Sh. Abdalla Farsy - Kadhi Mkuu/Kenya (1937-1947) - Babaake Prof Ali Mazrui
6.	Sh. Muhammad Kassim **Mazrui**	1912	1982	- Kadhi Mkuu/Kenya (1963-1967) - Babaake Prof Alamin Mazrui na Sh. Hammad M. Kassim (Kadhi Mkuu/Kenya (2002 - 2010)
7.	Sh. Abdalla Swaleh Farsy	1912	1982	- Kadhi/Zanzibar (1960-1967) - Kadhi Mkuu/Kenya (1968-1980)

Mahusiano na Mafungamano baina ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry na Sh. Muhammad Kassim Mazrui

Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** ni mjukuu wa Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry**. Mamaake Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** ni Bi. Khadija binti Muhammad Soud **Al-Maamiry**. Dadaake Bi. Khadija, Bi. Salma Muhammad Soud Al-Maamiry aliolewa na **Bw. Muhsin Muhammad Kassim Al-Maamiry**. Kwa hivyo Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** ni mjukuu wa Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry** kupitia kwa *Khalati* (*Aunty*) Bi. Salma Muhammad Soud Al-Maamiry. Akapewa jina la babu yake huyu, na *Alhamdu Lillah*! Jina likaswibu, kitabia na jaha, akachukua mwenendo hatua kwa hatua za somo yake.

	Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry	**Sh. Muhammad Kassim Mazrui**
Amezaliwa	Mjuakale, Mombasa – 1266 A. H. (1850)	Mjuakale, Mombasa - 1912
Amekufa	Mombasa – 26 Mfungo Tatu 1372 (9 January 1910); amekufa na umri wa miaka 62	Mombasa – 1982; amekufa na umri wa miaka 70
Kusoma kwake	Ameanza kusoma kwa babaake, Sh. Kassim Al-Maamiry. Baadae akaendelea masomo ya juu zaidi kwa Sh. **Ali b. Abdalla b. Naf'i Mazrui**	Ameanza kusoma kwa Sh. Ahmad Muhammad Matano. Baadae akendelea masomo ya juu zaidi kwa Sh. Al-Amin **b. Ali b. Abdalla b. Naf'i Mazrui**
Kazi za Dini	Darsa za nyumbani kwake na nyengine Msikiti wa Basheikh/ Mombasa	Darsa za nyumbani kwake na nyengine Msikiti wa Mazrui/ Mombasa
Kazi za Serikali	Kadhi na baadae Kadhi Mkubwa wa Mombasa	Kadhi wa Lamu, Malindi na baadae Kadhi Mkuu wa Kenya
Wanafunzi wake walokuwa Ma-Kadhi	Sh. Suleiman Ali Khamis Mazrui kama Kadhi wa Mombasa, na baadae akawa Kadhi Mkuu wa Kenya	Sh. Ali Mwenzagu kama Kadhi wa Mombasa; Sh. Ali Darani kama Kadhi wa Nairobi
Sifa Zake	Mwanchuoni aliesifika na Ucha-Mngu na mwenye haiba kubwa	Mwanchuoni aliesifika na Ucha-Mngu na haiba kubwa
Kuzikwa kwake	Katika makaburi ya Maamiry – Mgandini/Bondeni/Mombasa	Katika makaburi ya Mazrui – Ngomeni/Kibokoni/Mombasa

Kwa upande mwegine, mahusiano ya Sh. Muhammad Kassim Mazrui na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni:

- Sh. Muhammad **Kassim** Rashid Ali Naf'i Mazrui – ammi na shekhe wake akiwa ni Sh. Al-Amin Ali Abdalla Naf'i Mazrui.
- Sh. **Kassim** Rashid Ali Naf'i Mazrui akamuoa Bi. Khadija Muhammad Soud Al-Maamiry – dadaake Bi. Salma Muhammad Kassim Al-Maamiry.
- Sh. Rashid Ali Naf'i Mazrui ni binamu wa Sh. Ali Abdalla Naf'i Mazrui.
- Wote wawili, Sh. Rashid Mazrui na Sh. Muhammad al-Maamiry ni wanafunzi wa Sh. Ali b. Abdalla, uhusiano wa kidugu, kuoana na kimasomo.
- Wote wawili walirithi U-Kadhi wa Sh. Ali b. Abdalla, kwani Sh. Ali b. Abdalla Naf'i alikuwa Kadhi wa Mombasa 1856-1870
    - Sh. Rashid b. Ali Naf'i nae akashika U-Kadhi 1870-1875
    - Sh. Muhamad Kassim Al-Maamiry akashika U-Kadhi 1875-1910

Utoto na Kusoma kwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alizaliwa Mombasa mwaka wa 1266 Hijria, sawa na 1850.

Sh. Al-Maamiry alianza masomo yake kwa babaake, Sh. Kassim b. Said Abdalla Al-Maamiry aliyekuwa Sheikhe wa Ki-Ibadhi. Kwa hivyo Sh. Muhammad alikulia kama Ibadhi, katika maeneo ya kwao Madobini, Mjuakale, Old Town, Mombasa

Wakati huo Sheikh aliyekuwa akivuma ni Sh. Ali b. Abdalla b. Naf'i Mazrui, aliweka Darsa zake katika Msikiti wa Basheikh, katika maeneo ya Kibokoni, Old Town, Mombasa. Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kwa hamu kubwa alokuwa nayo juu ya kujiendeleza kielimu, hakuweza kuzuilika kwenda katika darasa za Sh. Ali b. Abdalla. Ikawa anakwenda kwa kujificha na kwa kuibia, kwa sababu Mzee wake hakupendelea mwanawe ende akasome kwa Sh. Ali b. Abdalla. **Si kwa kuwa baba mtu hakumuheshimu Sh. Ali b. Abdalla,** bali khofu yake kubwa ni kwa mwanawe kubadili Madhehebu yake ya ki-Ibadhi na kumfuata Sh. Ali b. Abdalla na kuwa Shafi.

Sh. Ali b. Abdalla kama alivyokuwa Sh. Muhammad b. Kassim Al-Maamiry, alizaliwa katika Madhehebu ya ki-Ibadhi kama walivyokuwa Mazrui wote wakati huo. Walakin, baada ya Sh. Ali b. Abdalla kufuatana na babaake, Sh. Abdalla b. Naf'i mwaka wa 1837, na wakenda zao kwa masomo mji wa Makka, Sh. Abdalla na mwanawe Sh. Ali waligeuza Madhehebu yao ya ki-Ibadhi na kufuata Madhehebu ya walimu wao wa Makka na kuwa ma-Shafi. Na kutoka Sh. Ali b. Abdalla aliporudi kwao Mombasa, akaanza kuvutia watu, hasa wanafunzi wake, wakafuata Madhehebu ya ki-Shafi. Hii ndiyo ilokuwa hofu ya Sh. Kassim b. Said Al-Maamiry juu ya mwanawe. Kwa hivyo baba mtu ikawa hapendi mwanawe kwenda kusoma kwa Sh. Ali b. Abdalla, asije akabadilishwa na kuwa Shafi.

Bidii ya mja haikidhi haja! Sh. Muhammad Kassim ikawa anaibia na kuhudhuria darasa za Sh. Ali b. Abdalla. Katika kunyapa-nyapa kwake huku, na kumkimbia babaake ili asijue kuwa anahudhuria darasa hizo, siku moja akaumwa na nyoka. N'gombe akivunjika guu, hukimbilia zizini. Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akiwa bado ni kijana, ikawa hana budi ila kukimbilia nyumbani kwa wazee wake. Akachechea mpaka nyumbani na kueleza maswaibu yalompata. Baba mtu akamtoa mwanawe sumu ya nyoka, akamuombea dua na kumpaka mwanawe mate ili kuyapoza machungu ya meno na sumu ya nyoka.

Baadae akamuuliza mwanawe, "Wewe si nilikukataza usende kwenye darasa za Sh. Ali b. Abdalla? Sasa unaona unavyo jihatarisha mpaka ukaumwa na nyoka?" – Asiesikiza la mkuu huvunjika guu! Kheri hutoka katika tumbo la shari! Baba mtu kwa kuwa na yeye pia ni Msomi, akaifahamu hamu ya mwanawe kufanya kila hila ili ayafuate masomo popote pale yalipo. Mwana yu tayari kujitia hatarini, ili apate nafasi ya masomo. Juu ya kuwa alikuwa mwana mtiifu, walakin shauku ya masomo ilimfanya kwenda kinyume na matakwa ya babaake. Si kwa kuwa alikusudia kuikengeuka amri ya babaake, walakin yeye hakuona ubaya wa kusoma kwa Sh. Ali b. Abdalla, wala hakuiogopa hatari ya kubadili Madhehebu. Na hivi ndivyo anavyosema Allah katika Surat Luqman 31:14-15

وَوَصَّيْنَا ٱلْإِنسَٰنَ بِوَٰلِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُۥ وَهْنًا عَلَىٰ وَهْنٍ وَفِصَٰلُهُۥ
فِى عَامَيْنِ أَنِ ٱشْكُرْ لِى وَلِوَٰلِدَيْكَ إِلَىَّ ٱلْمَصِيرُ ﴿١٤﴾

وَإِن جَٰهَدَاكَ عَلَىٰٓ أَن تُشْرِكَ بِى مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ فَلَا
تُطِعْهُمَا ۖ وَصَاحِبْهُمَا فِى ٱلدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۖ وَٱتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ
إِلَىَّ ۚ ثُمَّ إِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

Surat Luqman 31:14 *Na tumemuusia mwanadamu juu ya wazazi wake wawili! Mamaake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. Basi: "Nishukuru Mimi (Mola wako, na uwashukuru) wazazi wako. Na Kwangu Mimi ndiyo marudio".*

31:15 *"Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na yale ambayo huna ujuzi nayo, basi usiwatii. Lakini kaa nao kwa wema hapa duniani,* ***nawe ishike njia ya yule anaelekea Kwangu****. Kisha marejeo yenu ni Kwangu Mimi, na Mimi nitawaeleza yale mliyokuwa mkiyatenda (duniani)".*

Changamoto ya masomo ya halali ya kidini ilimruhusu mwana kukengeuka katazo la baba na kuifuata haki. Na baba nae ilipomdhihirikia hamu ya mwanawe ya kutaka na kuitafuta haki, na yeye akasalimu amri na kumruhusu mwanawe ende kwa Sh. Ali b. Abdalla na kuwa mwanafunzi wake kwa idhni yake.

Qadar ikatimia! Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akawa mwanfunzi mwema na hodari wa Sh. Ali b. Abdalla, nae Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akawa ndie naibu wa Sh. Ali b. Abdalla. Akapata ijaza ya Shekhe wake na akawa mfuasi kamili wa Sh. Ali b. Abdalla - ki-elimu, ki-tabia, ki-Madhehebu, ki-Ucha Mngu na akawa ni mkono wa kulia wa Sh. Ali b. Abdalla

na kuzirithi kazi zake za Darsa ya Msikiti wa Basheikh na vile vile kazi ya Ukadhi wa Mombasa. Na bahati kubwa aloipata ni kuwa Mwalimu na Sheikh wa wanafunzi wenzake kama Sh. Suleiman b. Ali b. Khamis Mazrui ambae nae alipata bahati ya kuzishikilia darasa za Sh. Ali b. Abdalla huko Pemba – Zanzibar wakati Sh. Ali b. Abdalla aliposhikwa na kufungwa na Sayyid Barghash. Sh. Ahmad Muhammad Mlomry, Mwanfunzi-mwenza wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry nae vile vile akaendelea kusoma chini ya Mwanafunzi mwenzake alipochukua usukani wa Shekhe wao.

Wanafunzi hao walosoma pamoja chini ya Sh. Ali b. Abdalla na kuendelea kusoma chini ya mwanafunzi mwenzao, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, na wao pia wakawa Ma-Ulamaa na kuzalisha Ma-Ulamaa. Kwani mwanafunzi mkubwa wa Sh. Suleiman ni Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947), aliyeurithi Ukadhi Mkuu wa Kenya wa Shekhe wake, nae akazalisha Mwanachuoni Sh. Muhammad Kassim Mazrui (1812-1982), ambae pia aliushika Ukadhi Mkuu wa Kenya.

Na Mwanfunzi mkubwa wa Sh. Ahmad Muhammad Mlomry ni Sh. Abdalla Swaleh Farsy (1912-1982). Sh. Abdalla pia aliwahi kusoma kwa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui. Na yeye pia akaurithi Ukadhi Mkuu wa Kenya kwa mwanfunzi-mwenza, Sh. Muhammad Kassim Mazrui.

Bahati ya pili aloipata Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni kumsomesha babaake mwenyewe. Baba yule yule alieanza kwa kumsomesha mwana, kisha akajitahidi kumzuia mwana asisome kwa Sh. Ali b. Abdalla Naf'i. Na baada ya mwana kuwa *A'lim* akarudi kuwa mwalimu wa babaake. *Allahu Akbar wali-Lahil Hamd!*

Athari ya Ulamaa hujulikana kwa wanafunzi alozalisha. Kwa hivyo athari kubwa ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni kuzalisha wanavyuoni walozalisha wanavyuoni. Subhana Allah! Hichi ndicho cheo cha Sh. Muhammad Kasim Al-Maamiry. Amerithi jaha ya Sh. Ali b. Abdalla, nae akawarithisha wanafunzi wenzake. Na wao wakaiendeleza kazi hii tukufu na kuiendeleza Imani na elimu ya Dini yao – *Alhamdu Lillah!*

Kipaji Cha Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry

Allah anasema katika Surat Al-Baqara

يُؤْتِي ٱلْحِكْمَةَ مَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُؤْتَ ٱلْحِكْمَةَ فَقَدْ
أُوتِيَ خَيْرًا كَثِيرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّآ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٢٦٩﴾

> ***Al-Baqara 2:269*** *Allah humpa hekima amtakae; na yule aliyepewa hekima, bila shaka amepewa kheri nyingi. Na wala hawayakumbuki haya ila wale wenye akili.*

Alhamdu Lillah! Thumma Al-hamdu Lillah! Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alitunukiwa hekima nyingi, kwani alikuwa Mwanafunzi hodari, akawakia wenzake na kupandishwa daraja ya kuziendeleza Darasa za Sh. Ali b. Abdalla alipofariki 14th August 1894. Aliziendeleza Darsa za Sh. Ali b. Abdalla baada ya kufa Sh. Ali mwaka wa 1894 mpaka kufa kwake yeye mwenyewe 1910 – muda wa miaka 16. Mwanafunzi akawa Mwalimu wa wanafunzi wenziwe wakiwemo Sh. Suleiman Mazrui na Sh. Ahmad Mlomry. Kama alivyokuwa Shekhe wake, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry vile vile alisifika sana kwa uhodari na hekima kubwa sana katika kusomesha kwake na pia katika uamuzi wa kesi za kisharia zilizoletwa mbele yake kama Kadhi. Darsa kubwa za Sh. Ali b. Abdalla zilizorithiwa na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry zilikuwa zikifanywa Msikiti wa Basheikh, Mombasa. Masaa ya Darasa yakiwa baina ya saa moja asubuhi hadi saa tatu, na baada ya Swala ya Adhuhuri hadi saa tisa – masaa 4 kwa siku.

Kuonesha uhodari wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry:

1. Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Ukoloni ya Uengereza wakiwa ndio wasimamizi wa Ukanda wa Pwani, walishauriana ichaguliwe Kamati ya Wataalamu watakao weza kuweka misingi ya kisheria itakayo tumiwa kuanzisha Waqf. Baada ya mashauriano marefu, ikaamuliwa

kuwa wakatafute mtaalamu wa Ki-Islamu huko Misri (Egypt) kwa kujulikana kuwa Al-Azhar inazalisha wataalamu wengi wa Dini. Kabla ya kutolewa mjumbe kwenda Misri, ikadhihirika kuwa wanae Mtaalamu wa Kisharia mjini Mombasa. Mtaalamu aliyetambulika ni Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.

Kwa hivyo akaombwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry awemo katika Kamati ya Wataalamu waingie katika *Mshawara* wa kuweka mikakati ya kuanzishwa kwa Kamati ya Waqf (*Waqf Commission)*. Wakaingia kazini kuzungumzia njia zitakazotumiwa na kunakili misingi kamili ya kisharia ya kuendeshea Kamati ya Waqf. Vifungu vya Sharia vya Waqf vikakubalika na kutekelezwa katika Mwambao wa Pwani wa Afrika Mashariki katika mwaka wa 1900 na Sultan wa Zanzibar.

Kamati ya Waqf ikaanzishwa rasmi Zanzibar mwaka wa 1904, na nchini Kenya, Waqf Commissioners Act ikawa sharia tarehe 8 Juni 1951. Kamati ya Waqf ya Kenya ina Wana-Kamati wanane, mmoja wao akiwa Kadhi Mkuu wa Kenya. Juu ya kuwa kifungu cha Sharia juu ya Kamati ya Waqf ilikuwa Sharia rasmi miaka mingi baada ya kufa kwake, walakin ifahamike kuwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ndiye Mtaalamu Wa Sharia za Ki-Islamu aliyeianzisha misingi hiyo kabla ya kufa kwake 1910.

2. Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alishika Ukadhi wa Mombasa takriban kwa miaka 35, na kuwa Kadhi Mkubwa wa Mwambao wa Pwani katika muda huo. Hivi ni kusema pakiwa na Kesi za Rufaa huletwa kwake.

Kesi Ya Rufaa kutoka Unguja (ZNZ)

Wakati mmoja Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa safarini Unguja na akaelezwa kesi ya bibi mmoja ambae hakuridhika na uamuzi wa urathi wake uloamuliwa na Sayyid Ahmad b. Sumayt. Sheikh akatoa ushauri kuwa bibi huyo akate Rufaa. Itakapopelekwa kesi Mombasa, hapo ndipo atakapo kuwa na uwezo wa kuisikiza kesi hiyo vilivyo na kutoa uamuzi wake. Sayyid Ahmad b. Sumayt alipopata habari kuwa bibi yule hakuridhika na uamuzi

wake katika kesi hiyo, na kuwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ataweza kuisikiza Kesi ya Rufaa alifurahi sana. Furaha yake ni kuwa ikiwa alikosea katika uamuzi wake basi itakuwa ni wajibu wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kumkumbusha pale alipokosea ili dhima imuondokee. Imani yake ni kuwa, *Alkamalu Lillah* – Mkamilifi ni Allah. Vile vile anajua Qur'an inafunza kuwa,

نَرْفَعُ دَرَجَٰتٍ مَّن نَّشَآءُ ۗ وَفَوْقَ كُلِّ ذِى عِلْمٍ عَلِيمٌ

> ***Surat Yusuf 12:76*** *..... Tunawatukuza kwenye vyeo tuwatakao; na juu ya kila ajuae yupo ajuae Zaidi (Juu ya kila mwenye ilimu yupo mwenye kumzidi katika ujuzi.*

Kwa hivyo ikawa anawahimiza yeye jamaa wende kwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry. Kwa hivyo jamaa wa bibi huyo wakakata Rufaa na kesi ikapelekwa Mombasa kwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kama Kadhi Mkubwa wa Ukanda wa Pwani.

Syd. Ahmad b. Sumeyt kama Kadhi wa Unguja aliyeiamua kesi hiyo hapo mwanzo nae vile vile akaja katika Mahkama ya Mombasa. Bibi yule aliyekata Rufaa akafuatana na jamaa zake. Jaji Mzungu wa Mahkama ya Rufaa akamwona Syd. Ahmad amebeba vitabu vyake ili aweze kuvitumia kama istish'hadi ya pale alipoegemea katika uamuzi wake. Walakin Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry aonekana na tasbihi tu, akiendelea na dhikri zake. Jaji akaingiwa na wasi wasi, akamnon'goneza Sh. Muhammad na kumuuliza mbona yeye hana vitabu vyovyote? Sh. Muhammad akamtuliza Jaji, na kesi ikaanza kusikizwa.

Bibi Mrathi akajieleza kuwa amechuma mali yeye na mumewe. Bwana alipokufa, wasimamizi wa Urathi wakamnyima haki yake. Akakipeleka kilio chake kwa Kadhi. Nae katika uamuzi wake ikaonekana pia hakumpa haki yake. Hapo Syd Ahmad akaulizwa nae ajieleze katika hukumu yake aliegemea wapi? Katika Wakala wa Usia bwana alijieleza kuwa mali wamechuma yeye na Ahli yake. Ikafahamika kuwa mali ni ya Bwana na mfanya-biashara mwenza, Ahli. Kwa hivyo yeye amempa Bibi haki yake ya Urathi kama sharia inavyotakiwa, akisubiriwa Mfanya biashara Mwenza nae apewe haki yake.

Bibi ameshajieleza na Kadhi nae ashaifahamisha Mahkama juu ya uamuzi wake. Hapo Kadhi Mkubwa, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akauliza: "Hapana shaka kuwa wewe ni Hafidhil Qur'an?"
Syd Ahmad b. Sumeyt akajibu, "Naam!" Sh. Muhammad akaendelea kumuuliza Syd Ahmad. Katika ile safari ya Nabii Musa alipotoka Madyan akirudi kwao Misri alikuwa amefuatana na nani? Hebu tusomee Aya hizo. Syd Ahmad akasoma katika Surat Al-Qasas 28:29


فَلَمَّا قَضَىٰ مُوسَى ٱلْأَجَلَ وَسَارَ بِأَهْلِهِۦٓ ءَانَسَ مِن جَانِبِ
ٱلطُّورِ نَارًا قَالَ لِأَهْلِهِ ٱمْكُثُوٓا۟ إِنِّىٓ ءَانَسْتُ نَارًا لَّعَلِّىٓ ءَاتِيكُم
مِّنْهَا بِخَبَرٍ أَوْ جَذْوَةٍ مِّنَ ٱلنَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٢٩﴾

> ***Surat Al-Qasas 28:29*** *Basi (Nabii) Musa alipotimiza muda (wa Mapatano), akasafiri pamoja na Ahli Zake, akaona moto upande wa Mlimani, akawaambia Ahli zake, "Ngojeni, hakika nimeona moto; labda nitawaletea habari au kijinga cha moto ili mupate kuota moto."*

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akamuuliza Syd. Ahmad pale alipomaliza kuisoma Aya hiyo, "Jee nini makusudio ya Ahli katika Aya hiyo?" Akajibu kuwa Ahli hapa ni mke. Hapo hapo Syd. Ahmad akafahamu pale alipoteleza. Akamshukuru Sh. Muhammad sana na kumwambia, "Ama kweli nimeziona baraka za Sh. Ali b. Abdalla. Hakika nimeuona ukunjufu wa elimu yake. Kutoka alipokufa Sh. Ali sijawahi kuja kumzuru. Kwa hivyo amenivuta ili nije nilizuru kaburi lake na kumuombea Dua. Basi nakuomba unipeleke kwenye kaburi lake ili nimzuru na kumuombea Maghfira!"

Hivi ndivyo wanavyo heshimiana *Ma-Ulamaa*. Syd. Ahmad b. Sumeyt alifurahi kwa kutanabahishwa na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, akatambua ukundufu wa elimu na heshima yake pamoja na ile ya Shekhe wake, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui. Bibi yule akaipata haki ya Urathi wake.

Alhamdu Lillah! Na sisi tukafaidika na uamuzi ulotolewa pamoja na kuiona heshima baina ya *Ma-Ulamaa!*

Sifa za Mwanachuoni

- Kusema na kueneza ukweli unaotokana na utafiti, uchambuzi na uelewa wake kwa jamii bila ya kujali kama ukweli huo unawapendeza au unawaudhi baadhi ya watu au watu wote.
- Kuwajibika kwa Umma, yaani kuwa na Wajibu-Jamii (*social responsibility*). Mwanachuoni huwajibika kwa jamii sio kwa sababu anashurutishwa lakini kwa hiari yake, kutokana na uanazuoni wake, ndiyo maana halisi ya mwanachuoni.
    - Katika kutekeleza wajibu-jamii wake, mwanachuoni anaweza akajikuta yuko peke yake au katika kikundi kidogo sana cha watu ambao wanakubaliana naye.
- Hashangiliwi wala hatuzwi; anachukiwa na kufedheheshwa; anatukanwa na kusingiziwa uongo na hata kutishwa. Ndio maana mwanachuoni ambaye ana ujasiri wa kusema ukweli anajipalilia makaa na kuhatarisha usalama wake. Sifa hizi mbili zikiunganishwa na utaalamu na ustadi wa kisomi ndio zinazaa Mwanachuoni halisi wa aina ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.

Sifa za Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry

أَمَّنْ هُوَ قَٰنِتٌ ءَانَآءَ ٱلَّيْلِ سَاجِدًا وَقَآئِمًا يَحْذَرُ
ٱلْءَاخِرَةَ وَيَرْجُوا۟ رَحْمَةَ رَبِّهِۦ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِى ٱلَّذِينَ
يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٩﴾

Surah Az-Zumar 39:9 *Jee! Mwenye kumnyenyekea Mwenye-ezi-Mngu nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama, akiiogopa Akhera, na akitaraji rehema za Mola wake (ni kama yule anae*

mwomba Mola wake wakati wa shida na akamsahau wakati wa neema?) Sema: Je! Watakuwa sawa sawa wale wanaojua na wale wasiojua? Hakika wanao kumbuka (na kuwaidhika) ni (wale) watu wenye akili (nzuri).

- Uwekevu – Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa mwekevu (*very intelligent*). Wanafunzi wenzake wote walilitambua hili na ndio maana alipokufa Shekhe wao, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i, jukumu la kuzindeleza Darsa zake zilimuangukia yeye Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.
- Akhlaq bora – Sh. Muhammad alisifika kwa tabia bora, tabia ya heshima na murua.
- Ucha Mngu – Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alisifika kwa sifa ya ucha Mngu. Alikuwa na haiba kubwa sana, akijishughulisha na swala mbali mbali za Sunna pamoja na za Tahajjud. Akipenda sana kufunga swaum za Sunna, na kila wakati akiwa na Tasbihi yake, ulimi na moyo wake ukifungamana katika nyuradi mbali mbali.
- Ukarimu – Anapopokea mshahara wake haufiki nyumbani. Apita akitoa sadaqa kwa wale alowaona ni wahitaji zaidi kuliko yeye.
- Uadilifu katika maisha yake na katika kuhukumu kesi zinazopelekwa kwake katika Mahkama ya Kadhi.
- Ushujaa – hakuogopa kuisimamia na kuisema haki hata kama itamtia matatani. Aliwahi kufungwa kama vile alivyofungwa Shekhe wake, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i kama tutakavyoona mbele.

Ushujaa wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry na Sh. Suleiman Ali Khamis Mazrui walifungwa (kama alivyofungwa Shekhe wao, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i) kwa kusimamia haki.

Alikuja bibi mmoja kushitaki kwa Sh. Al-Maamiry kuwa anateswa na mumewe na kuomba aachishwe. Kama Sharia inavyohitaji, huwezi kuhukumu kesi kwa kusikiza upande mmoja, kwa hivyo mume akaitwa kuhojiwa, Bwana kwa kuwa anatoka katika ukoo wa kibepari uloshirikiana na Serikali ya

Ukoloni wa Kiengereza alimtolea Shekhe ufidhuli na kumwambia kuwa hatomuacha wala Kadhi hatoweza kufanya jambo lolote.

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa mtu wa hekima sana. Baada ya kushauriana na Sh. Suleiman Mazrui, mwanafunzi wake na Kadhi wake mdogo wa Mombasa, walimshauri bibi avae vazi litakalo mshawishi mumewe amuone ni kama mtu ambae ametoka katika dini, kisha ende akalitembelee kanisa. Bibi alifuata ushauri huo, na bwana juu ya jeuri alizokuwa nazo, walakin Imani ya dini ilikuwepo japo kidogo. Akashawishika kuwa maonevu na jeuri zake dhidi ya mkewe ndizo zilizompelekea mke kutoka katika Uislamu. Kwa hivyo yeye ndie sababu ya mkewe kuritadi. Hayo yalimuumiza sana na akawa hana budi ila kumuacha mkewe.

Kwa machungu na jeuri alizokuwa nazo, na kwa kutumia uhusiano wake na serikali ya kibepari, akawazunguka ma-Kadhi na kuwashtaki kuwa wamekula rushwa katika kesi yake na mkewe. Serikali ya Ukoloni kwa kupenda kuwagawanya raia zake kwa matapo mbali mbali, ili wawatawale na kuwagandamiza, waliwahukumu Ma-Kadhi wote wawili na kuwafunga gerezani kwa muda. Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry na Sh. Suleiman b. Ali Mazrui wakaifuata Sunna ya Nabii Yusuf (A.S.), wakafungwa kama alivyofungwa Shekhe wao, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui.

Kioo Cha Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry Kupitia Kwa Sh. Muhammad Kassim Mazrui

Kuna msemo unaokubalika kuwa mtu anapopewa jina la mmoja wa wazee wake waliotangulia, jina hilo huwa na athari kubwa sana kwa yule alopewa jina hilo. Kuna kusibu jina kwa njia hiyo na pia tukumbuke pia kuna na athari za tembe-tembe za uzazi (*genetics* – kwa njia ya *DNA*). Baada ya kufanya utafiti juu ya maisha ya Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry** na kuishi na Sh. Muhammad Kassim **Mazrui**, naona kuwa sitokuwa ni mwenye kutoka katika maudhui ya Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry** ikiwa nitaeleza namna gani mjukuu wake huyu alivyo zivaa baadhi ya tabia zake.

Kwa hivyo ningependa kuzitumia sifa nilizo muona nazo Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** kama kioo cha kumtizama na kuzitathmini sifa na mwenendo wa Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry**. Kama nilivyotangulia kusema katika *"Mahusiano na Mafungamano baina ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry na Sh. Muhammad Kassim Mazrui"* hapo mbeleni katika kitabu hiki kuwa Sh. Muhammad Kassim Mazrui alipewa jina la babu yake, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry. Nikasema kuwa jina likaswibu, kitabia, jaha na kumfuata babu yake huyu hatua kwa hatua.

Kwa kuwa tumemuona na kuishi na Sh. Muhammad Kassim **Mazrui**, tunaweza kuchukua ruwaza kutoka kwake na kumtumia kama kioo ama darubini ya kummulika na kuzitathmini sifa za Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry**.

Zifuatazo ni sifa nilizoziona mimi mwenyewe:

- Mwendo wa utaratibu katika kutembea kwake. Akitembea wima na kwa staha, ukiziona khatua zake thabiti, ukiuona upole wa ushujaa na haiba katika mwendo wake. Na hivi ndivyo anavyowasifu Allah waja Wake wa kweli,

  وَعِبَادُ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى ٱلْأَرْضِ
  هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ ٱلْجَٰهِلُونَ قَالُوا۟ سَلَٰمًا ﴿٦٣﴾

  Surat Al-Furqan 25:63 *Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!*

  Sayyid Qutb katika Tafsiri yake *Fi Dhilalil Qur'an* [Katika Kivuli Cha Qur'ani] alipokuwa akiieleza Ayah hii, anasema:

  Sifa ya kwanza ya mja wa Mwenye-ezi-Mngu ni kuwa hutembea kwa staha, bila ya madaha, majivuno, wala kiburi. Kama ilivyo katika kila mwenendo wa mwanadamu, namna anavyotembea hufichua tabia, umbile na hisia za mtu yule. Khulka ya ukakamavu

ilio thabiti na utulivu hujulikana kwa namna mtu anavyotembea. Mtu wa aina hii hutembea kwa hatua tulivu thabiti, zinazodhihirisha uwazi katika kusudio na ushuja wake. ***Kutembea kwa staha*** *hakumaanishi kuwa Waumini wa Kweli hutembea kigoigoi na kwa masikitiko kama wanavyodhani baadhi ya watu kuwa tabia ya kujitweza ndio Ucha-Mngu. Mjumbe wa Allah (Nabii Muhammad, S.A.W.) alikuwa mwepesi katika matembezi yake, akiinamia upande wa mbele yake. Alikuwa akitembea kwa hatua bora za haraka haraka, zilizo tulivu.*

Abu Huraira (A.S.) katika kuusifu mwendo wa Mtume (S. A. W.) anasema: "Sijawahi kuona mtu mwengine yoyote aliye jamali kuliko Mjumbe wa Allah. Utadhani mwangaza wa jua una nawirisha uso wake. Sijawahi kuona mtu aliyekuwa akitembea haraka haraka kuliko Mjumbe wa Mwenye-ezi-Mngu. Ilikuwa ni kama ambae ardhi ikijikunja kwa ajili yake. Tunapotembea nae, tulijikakamua na kujikaza sana kwenda sambamba na yeye, walakin ajabu ni kuwa yeye alikuwa mtulivu katika hatua hizo.

- Vazi lake lilikuwa ni kanzu, kikoi, juba na kilemba. Kilemba chake kikiwa na kishali kilicho angukia upande wa kulia. Tizama picha yake mwisho wa kitabu hiki.
- Haiba ya Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** ilikuwa ya hali ya juu sana. Ukiwa mbele yake unakaa kwa heshima na adabu. Hata wale walokuwa wakimpinga, wakisemea kwa mbali. Alikuwa na utisho wa kiheshima wa ajabu!

Mara moja akinihadithia yeye mwenyewe: Alikuwa safarini kwa gari la moshi (*train*) kwenda Nairobi wakati akiwa Kadhi Mkuu. Vyumba vya *1st Class* vilikuwa ni watu wawili wawili. Safari ya *train* aghlabu ikianza saa kumi na mbili unusu jioni.

Alipoingia chumbani aliona ishara kuwa tayari mwenziwe ameshatangulia kuingia, walakin hakuwemo chumbani wakati huo. Saa za kuondoka *train* ikiwa tayari magharibi imesha ingia. Kwa

hivyo akatandika mswala wake na kuswali. Akiwa ndani ya swala, akahisi mlango ukifunguliwa na karudishwa pole pole na kufungwa.

Sh. Muhammad Kassim akaendelea na swala zake. Alipomaliza akapanda kitanda chake na kujipumzisha. Yule mwenziwe akampa muda wa kutosha, hakurudi chumbani ila baada ya kukinai kuwa sasa Sheikh atakuwa ameshamaliza swala zake. Yule mwenziwe kumbe alikuwa ni Kalasinga (*Sikh*). Kwa haiba aliyo muona nayo Sh. Muhammad, bwana yule aliingia chumbani kwa heshima kubwa sana. Baada ya kusalimiana, Kalasinga yule hakuwa na mazungumzo yoyote. Akaingia na adabu, na kumwekea Sh. Muhammad heshima sana na kukaa kwa adabu na utulivu. Kila mmoja akawa juu ya kitanda chake bila ya kuudhiana, mpaka wakafika Nairobi na kuagana kwa upole na salama.

- Sh. Muhammad Kassim Mazrui alikuwa akifanya kazi ofisi yake akiwa kama Kadhi Mkuu ikiwa hapo *Treasury Square*. Akiishi Kibokoni, wakati huo nyumba yake ikiwa karibu na Msikiti wa Azhar (maarufu, Msikiti wa Mwalimu Alii). Basi baina ya ofisi na nyumbani, Sheikh Muhammad alikuwa akifuata barabara ya *Ndia Kuu*. Kwa kuchunga haiba yake, heshima yake haikumpa kupitia njia za mkato mitaani. Akifuata njia ya magari! Hakupenda kupita mbele ya milango ya mitaani. Akijiheshimu na watu wakimuheshimu.
- Kila baada ya muda fulani alikuwa akija nyumbani kwetu kuja kumtembelea Mkwewe, Bi. Swafia binti Suleiman Mazrui (*MaBilee*). Bi. Swafia ndiye Mama Mkwe na pia ndiye mke wa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui, Mwalimu/Shekhe wake Sh. Muhammad Kassim Mazrui. Kabla ya kuja, Sh. Muhammad hutuma salamu kwanza kuwa anataka kuja kumtembelea Bi. Swafia. Hii ndiyo heshima ya kutembeleana. Hakutaka kuja bila ya taarifa. Alipendelea ijulikane mapema kuwa atakuja, sio kufika bila ya taarifa.

  Kwa hivyo alimpa Mkwewe muda wa kutosha kujitayarisha. Ifahamike kuwa wakati huo Bi. Swafia ni mzee. Wote, mtu na Mkwewe wakiwekeana heshima ya hali ya juu sana. Na sisi wajukuu tukifunzika na kupata ruwaza baina ya Khali, Sh. Muhammad Kassim

na bibi, Bi. Swafia. Unafunzika kwa kuona heshima na mapenzi yaliokuwepo baina ya mtu na Mkwewe – *Alhamdu Lillah*.

- Darsa kubwa za Sh. Muhammad Kassim zilikuwa Msikiti wa Mazrui. Wanafunzi watu wazima walikuwa wengi. Kila mmoja akija mapema pamoja na kitabu chake. Prof Alamin wakati huo bado ni kijana, akifika mapema na kumtayarishia babaake *Marfaa* na kumwekea vitabu vyake.

  Sh. Muhammad anapoingia uone utulivu ulivyo tanda Msikitini. Wazee kwa vijana wakiwa wametulia kwa heshima na adabu.

  Sisi watoto tukitulizana bila ya kujitambua kuwa tumekaa kwa utulivu. Hii ndiyo haiba alokuwa nayo Sh. Muhammad. Utisho wa kiheshima kwa wote waliokuwepo mbele yake.
- Darasa nilizo ziona nyumbani ni za Ma-Kadhi. Sh. Ali Mwenzagu na Sh. Ali Darrani, kila mmoja akija kwa wakati wake. Kila mmoja atakuja na kitabu chake, asomeshwe kwa ule muda alowekewa. Hapa ndipo nilipojua faida ya kupiga goti na kusoma kwa Shekhe wako. Upate somo, utulivu na *Akhlaq* kutoka kwa Shekhe wako. Na anapotosheka na wewe, Shekhe wako anakuandikia *Ijaza* (Shahada).

  Bahati mbaya ni kuwa leo usomeshaji kama huu si rahisi kupatikana. Wengi katika wasomi wetu wana Shahada za Vyuo Vikuu, walakin hawana *Ijaza* ya *Ma-Ulamaa*.

  Alhamdu Lillah! Katika **RIS CONVENTION** inayofanyika kila mwaka huko Toronto, Canada, unao andaliwa na vijana wa Ki-Islamu, ni Muhadhara wa siku tatu. Huwaalika Ulamaa kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu ili waje watoe fikra zao na mafunzo ya kuwashajiisha vijana wa leo wafaidike na kuzichemsha Imani zao juu ya Dini ya Ki-Islamu. RIS kwa urefu ikiwa ni **Revival of the Islamic Spirit** – Ingia kwenye mtandao http://risconvention.com/.

  Baada ya Muhadhara wa takriban watu 20,000 huwepo na **KNOWLEDGE RETREAT** - http://risconvention.com/knowledge-

retreat/. Huu ni wakati wa kupiga goti mbele ya ma-Ulamaa waliopo na upate uhondo wa namna wanavyo someshwa Wasomi wa Dini.

Huu ufuatao ndio muhtasari katika mtandao wa RIS CONVENTION juu ya walivyo kuwa wakisoma na kupokea Ijaza:

> ***KNOWLEDGE RETREAT*** *28th December, 2015 ~ 2nd January, 2016*
>
> *Reviving the Islamic Spirit Knowledge Retreat is an annual program held around the RIS Convention to give seekers of knowledge an opportunity to study traditional Islamic sciences, in contemporary context, with some of the leading scholars of our time. Knowledge is the greatest gift a believer can share and it is through such gatherings that students are introduced to the depth and breadth of Islamic scholarship. Rarely do Muslims living in the west get such opportunities and hence RIS KR strives to provide a conducive environment for students to purse their quest for knowledge and enlightenment by studying the traditional sciences preserved through a chain of transmission handed to us through great scholars of the past.*
>
> ***Kuhuisha Moyo wa Ki-Islamu – Kikao Tulivu Cha Elimu****, ni kikao maalum kinacho fanywa kila mwaka baada ya Muhadhara wa RIS CONVENTION na kuwapa nafasi watafutao elimu ukumbi wa kujifunza kama vile walivyokuwa wakisomeshwa wanafunzi wa tangu jadi "Sayansi ya Mafunzo ya Ki-Islamu". Ukumbi huu unaendeshwa na Wasomi wetu wakuu wa leo. Elimu ni hidaya kubwa anayoweza Muumin kumtunukia mwenziwe. Na ni katika vikao kama hivi ndipo wanafunzi wanaweza kupata wasaa wa kutambua na kufahamu vina virefu na mapana vya Usomi wa Ki-Islamu. Ni vigumu kwa wale wanaoishi katika nchi za Magharibi kupata fursa kama hii.*

*Na ndio maana **Kikao Tulivu cha Elimu** cha RIS huandaa mazingira ya kufana kwa wanafunzi kufuatilia na kunufaika na masomo kwa njia za jadi zilizo hifadhiwa kupitia kwa Ulamaa wa kale.*

- Sifa za Ucha-Mngu (*Taqwa*) wa mtu ni vigumu kwa mja mwengine yeyote kuzisimulia, kwani Mtume (S.A.W.) ameshatueleza kuwa *Taqwa* iko moyoni. Tunayoweza kusimulia ni yale mambo yanayodhiri katika umbile na mwenendo wa mtu. Nikirudia kutoa wasifu wa Sh. Muhammad Kassim Mazrui kama kioo cha kumuangalia Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni ile sifa ya Ucha-Mngu.

  Nimewahi mara nyingi kuswali nyuma ya Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika Msikiti wa Mazrui na vile vile kama nilivyo tangulia kutaja katika utangulizi, kuswali tukiwa wawili tu chumbani kwake. Nime shuhudia utulivu wa swala zake akiwa yeye ndiye Imamu na pia kama Maamuma katika Swala ya Ijumaa katika Msikiti wa Basheikh na ya Tarawehe katika Msikiti wa Mazrui. Utamuona Sh. Muhammad ametulia kwa unyenyekevu ndani ya swala.
- Mtulivu katika kuzungumza na kukupa nafasi ya kusema bila ya kukuharakisha au kukubabaisha. Na anapokujibu uone utulivu na upeo wa kipawa cha fikra na elimu. Haogopi kukupa ukweli, na anapokupa ukweli katika jawabu zake unatosheka na unahisi dhati ya funzo analokupa.
- Sh. Muhammad hakuogopa kuitetea haki hata ikiwa haki hiyo itamtia matatani. Na haya yanadhihirika wazi katika vitabu vyake na gazeti lake la *Sauti ya Haki*. Vitabu hivyo mpaka leo bado vinatafutwa na kusomwa kwa wale wanaotaka haki.
- Ukakamavu katika uamuzi wa kesi zilizoletwa mbele yake. Na Ukakamavu katika kutoa *Fatwa* inapohitajika.

  Kenya Meat Commission (KMC) walipoanza kutumia *sten-gun* ya kuwapiga n'gombe risasi ya ganzi ili kurahisisha katika kuchinja, palizuka utesi mkubwa Mombasa. Ushindani ukawa, jee yafaa

kupigwa n'gombe risasi ya ganzi au haifai. Ushindani ulipozidi Sh. Muhammad akenda KMC kwenda kujionea mwenyewe kile kinachofanywa kabla n'gombe hawajachinjwa. Alipotosheka akatoa *Fatwa* yake kuwa hamna kosa lolote na kuwa nyama hizo ni halali kuliwa. Hakusema tu, bali na yeye akatangulia kula nyama hizo zinapopikwa. Nyama hizo pia zikatumiwa kupikia sambusa na kababu na kukaribishwa wale walokwenda kumtembelea nyumbani hasa siku za Eid. La ajabu ni kuwa wale walokuwa wakipinga, walikuwa ni moja ya wale walokuwa wakimtembelea kwa heshima walokuwa nayo juu yake. Na wanapokaribishwa vitamu hivyo hawakuvikataa. Haya si mambo niloyasikia, bali ni mambo niliyo yashuhudia mwenyewe – mimi nikiwa ni mmoja kati ya watoto wa nyumbani kwa Sh. Muhammad. **Utesi wa kutumiwa kwa *sten-gun* ukesha!**

- Ushujaa huu na mchango wa Sh. Muhammad Kassim Mazrui nimepokea kutoka kwa Sh. Hammad:
    - Sh. Muhammad Kassim Mazrui na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry mbali na kuwa walikuwa *Ma-Ulamaa* wa Kidini, walakin pia walikuwa watetezi wakubwa wa kuhifadhi Mila na Murua (*culture*) pamoja na kuwa msitari wa mbele katika kuutetea uhuru na haki zetu za kisiasa, kisharia na njia halali za kutafutia maisha – (*advocates of our culture, and fighters of our political as well as economic rights*).
    - Wakati kulipokuwa na njama za kuwagawanya Wa-Islamu wa Wapwani ya Kenya kwa makundi ya kikabila - Waaarabu, Wahindi na Waafrika (*divide and rule*), Sh. Muhammad Kassim Mazrui aliwaita viongozi nyumbani kwake ili wapange mikakati ya kutokubali kugawanywa kikabila.
    - Vile vile wakati wa mijadala ya kuwataka Wa-Islamu wa Kenya wasahau Sharia zao juu ya Urathi na kufuata Sharia moja ya nchi juu ya Urathi (*The Law of Succession*), Sh. Muhammad aliweza kuwashajiisha viongozi wa ki-Islamu, wa ki-Dini na ki-Siasa. Akaweza kuwapa hoja nzito za kuweza kushinda majadiliano hayo na kifungu hicho cha Sharia kutupiliwa mbali, Wa-Islamu wakapata afueni.

— Ingawa Eidul Fitri ilikubaliwa kuwa Siku Kuu nchini Kenya wakati wa Sh. Abdalla Swaleh Farsy, walakin barua ya maombi aliyoikabidhi Sh. Abdalla Serikalini ilipangwa na (*drafted by*) Sh. Muhammad Kassim Mazrui.

- Wakati wa kufa kwake, Allah alimsahilishia sakarati yake! Nimempokea Al-Akh Gharib Muhammad Kassim Mazrui kuwa, siku zote Sh. Muhammad Kassim Mazrui alikuwa akimuomba Allah kuwa katika uzee wake na kufa kwake amsahilishie ili asiwape taabu watu wake kumuuguza. Sh. Muhammad alikufa nyumbani kwa mkewe wa pili huko Kisauni – kwa mamaake Sh. Hammad Muhammad Kassim. Baada ya kuswali Swala ya Alfajiri, Sheikh alisema kuwa hajisikii vizuri. Akaingia chooni, akamaliza haja zake, akatawadha na kurudi kitandani kulala. Bibi nae akarudi kitandani kujipumzisha.

  Wakati wa Sakarati aliwahi kuunyosha mkono wake na kumshika mkewe. Hapo bibi akashutuka na kumuona mumewe akihangaika. Alhamdu Lillah! Bi. Salma na binti yake, Bi. Sauda Muhammad Kassim Mazrui, Mwenye-ezi-Mngu aliwapa taufiki na kuwahi kumpa Sh. Muhammad Kassim vijiko viwili vitatu vya maji. Hapo tena Sh. Muhammad Kassim akasallim amri na kuungana na babu yake kipenzi, Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry katika *Barzakh*. Mwenye-ezi-Mngu awaghufirie na kuwalipa Jannatul Firdaus kwa kazi kubwa walizofanya juu ya Dini - Amin.

  Ndugu Gharib anahadithia kuwa kama saa moja unusu asubuhi, alipata simu kutoka kwa dadaake, Sauda Mazrui, akimweleza hali ya baba yao kuwa imebadilika – bila ya kumshutua kuwa kuwa mzee ameshafariki. Gharib akamfuata kakaake, Bw. Munir Mazrui na wakafanya haraka kwenda Kisauni. Wakifika wakamkuta baba yao ameshakufa. Wakatafuta daktari aliye karibu ili ahakikishe kufariki kwa baba yao. Daktari alipofika na kumtizama kwa vipimo vya kidaktari, akawatangazia kuwa kweli mzee ameshafariki. *Alhamdu Lillah!* Sh. Muhammad alifikiwa na mauti kama alivyokua akiomba.

Allah akamtakabalia Dua yake, na roho yake kuchukuliwa na *Malakul Maut* bila ya kuwahangaisha watu.

إنا لله وإنا إليه راجعون

Karama za Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry

Moja katika Aya alizokuwa akizipenda sana Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry ni:

وَمَن يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَل لَّهُ مَخْرَجًا
وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ

Surah At-Talaq 65: 2-3 *.... Na anaye mcha Mwenye-ezi-Mngu, basi (Allah) humtengenezea njia ya kutokea (katika kila dhiki). Na humruzuku kwa njia asiyo itazamia...*

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa akiikariri Ayah hii mara kwa mara. Na labda ndio maana pale anapopokea mshahara wake alikuwa akiutoa sadaqa. Mshahara wake haukua ukifika nyumbani! Twaweza kuutumia mfano wa Sayyidna Abubakar As-Siddiq (R.A.) pale Mtume (S.A.W.) alipowataka Maswahaba wachangie katika kulitayarisha jeshi la Mtume la kwenda kupigana Jihadi. Kila Swahaba alijitolea kwa kile alichoweza. Alipokuja Sayyidna Abubakar (R.A.) kuleta mchango wake, aliulizwa na Mtume (S.A.W.), “Jee umewabakishia nini watu wako wa nyumbani?” Jibu lake likawa, “Nimewaachia Allah na Mtume wake!”

Sh. Muhammad Kassim kwa hivyo alikinai kuwa Mwenye-ezi-Mngu ndiye anae mruzuku yeye pamoja na familia yake.

Jambo la pili: Yayumkini kuwa hakupenda kuzifikisha pesa za Serikali katika nyumba yake. Huenda aliziona kuwa pesa hizo hazitokamani na njia za halali

tupu. Kwa hivyo hakupendelea kula yake na ya familia yake iwe inatokana na fedha ambazo si safi. *Allahu a'alam* – (Allah ndiye ajuae)!

Jee riziki yake ilikuwa ikitoka wapi, ikiwa pesa anazozipata za mshahara wake sizo alizokuwa akitumia? Hapo ndipo riziki ya Mwenye-ezi-Mngu inapokufikia kwa njia anazopenda Mwenyewe Allah. Kwa hivyo tutatoa mfano mmoja kuonyesha namna Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alivyokuwa akiishi.

Mara moja akiwa Barazani kwake nyumbani, jamaa zake walipokuwa wakijitayarisha kupika chakula cha mchana, walimuuliza, "Mzee hakuna kitoweo leo." Sheikh akajibu bila ya kusitasita, "Hebu tizameni katika birika." Jamaa wakitizama katika hodhi wakakuta samaki anaogelea, na ilihali hamukuwa mukifugwa samaki nyumbani. Kitoweo kikapatikana na jamaa wakatayarisha chakula.

Hili si ajabu. Kwani Bibi Maryam alikuwa akiruzukiwa na Allah kama anavyotueleza Allah katika Qur'an,

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٍ وَأَنۢبَتَهَا نَبَاتًا حَسَنًا وَكَفَّلَهَا زَكَرِيَّا ۖ
كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيۡهَا زَكَرِيَّا ٱلۡمِحۡرَابَ وَجَدَ عِندَهَا رِزۡقًا ۖ قَالَ يَٰمَرۡيَمُ
أَنَّىٰ لَكِ هَٰذَا ۖ قَالَتۡ هُوَ مِنۡ عِندِ ٱللَّهِ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ يَرۡزُقُ مَن يَشَآءُ بِغَيۡرِ
حِسَابٍ ٣٧

Surah Al'Imran 3:37 *Tena Mola wake Mlezi akampokea kwa mapokeo mema na kumkuza makuzo mema, na akamfanya (Nabii) Zakaria awe mlezi wake. Kila mara (Nabii) Zakaria alipoingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimuuliza, "Ewe Maryam! Unavipata wapi (vyakula hivi)?" Nae akajibu, "Hivi vinatoka kwa Mwenye-ezi-Mngu; na Mwenye-ezi-Mngu humruzuku amtakae bila ya hesabu."*

Urithi (Legacy) Wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry

Kama alivyosema Sh. Abdalla Swaleh Farsy katika kitabu Chake *"Baadhi ya Wanavyuoni wa KiShafi wa Mashariki ya Afrika"* kuwa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry anakumbukwa kwa mambo mazuri aliyayaacha. Tutaje kwa muhtasari baadhi ya mambo yaliodhihirika ili tutathmini Urithi wake:

1. Wanafunzi waliondeleza kazi alizorithi, akazikuza kisha akazirithisha
   - Sh. Suleiman b. Ali Khamis Mazrui, akianza kama Mwanafunzi-Mwenza wakiwa pamoja chini ya Sh. Ali b. Abdalla Naf'i. Baadae akawa mwanafunzi wake na baadae kuendeleza Darsa. Yeye akazihamisha Darsa kutoka Msikiti wa Basheikh alipowaachia wenzake waendeleze huko, na yeye kuanzisha Darsa hizo Msikiti wa Mazrui.
     - Vile vile Sh. Suleiman Mazrui alikuwa Kadhi Mdogo wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kwa miaka kadha. Akaendelea kuwa Kadhi Mdogo wa **Sayyid Abdurahman bin Ahmad bin Umar Al-Saggaf (Mwinyi Abudu, 1833-1922)** aliye chaguliwa kuwa *Shekhul Islam* 1902-1922.
     - Sh. Suleiman Mazrui akawa Kadhi Mkuu wa Kenya (1932-1937). Hii ni baada ya Sh. Mohammad bin Omar Bakore kujiuzulu kama Chief Kadhi wa Kwanza mwaka wa 1932. Cheo cha Sheikhul Islam kilibadilishwa na kuwa Chief Kadhi.
     - Sh. Suleiman Mazrui akazalisha *Alim* alie endeleza kazi za Darsa na Kadhi Mkuu wa Kenya baada yake. Sh. Al-Amin Mazrui akashika kazi hiyo ya Kadhi Mkuu 1937-1947.
     - Nae Sh. Al-Amin Mazrui akazalisha Ulamaa alie endeleza kazi za Darsa na Kadhi Mkuu wa Kenya baada yake, Sh. Muhammad Kassim Mazrui akawa Kadhi Mkuu kuanzia 1 May 1963 hadi 1967.
     - Sh. Muhammad Kassim Mazrui alikufa 5 April 1982
   - Sh. Ahmad Muhammad Mlomry nae pia alikuwa Mwanafunzi-Mwenza wa Sh. Muhammd Kassim Al-Maamiry na baadae kuwa mwanfunzi wake kama alivyokua Sh. Suleiman Mazrui.

— Sh. Mlomry nae akazalisha *Alim* aliyefuata hatua za Ma-Shekhe wake. Sh. Abdalla Swaleh Farsy akaendeleza Darsa na Ukadhi na baadae kuwa Chief Kadhi wa Zanzibar 1960-1967.
— Sh. Abdalla Farsy kustaafu Sh. Muhammad Kassim Mazrui akawa Chief Kadhi wa Kenya 1968-1980.
— Sh. Abdalla Farsy alifariki Muscat 9 November 1982.

2. Mwana na wajukuu walofuata hatua za Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.
   - Bw. Muhammad b. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa Wakili wa Ki-Islamu. Jina maarufu akiitwa Sh. Badi. Yeye ndiye aliye andika Mashairi ya Kaswida ya "Muadda Muadda Ya Ramadhan".
   - Mjukuu aliyechukua jina, jaha na kazi ni Sh. Muhammad Kassim Mazrui – kama tulivutangulia kumueleza.
   - Mjukuu wa pili ni Sh. Al Amin b. Muhsin Muhammad Kassim Al-Maamiry aliyezaliwa 1928. Mjukuu huyu amesoma kwa Sh. Al-Amin Mazrui, Sh. Muhammad Kassim Mazrui, Sh. Rashid Mazrui, Sh. Abdalla Ali Maawy, Syd. Ali Ahmad Badawy na pia kwa Syd. Ahmad Taha Al-Haddad. Sh. Al amin alichaguliwa kuwa Kadhi wa Kisumu 1972.
   - Kilembwa anaefuatilia kazi za uwakili ni Aisha Salim Ahmad Muhsin. Inaonekana tembe tembe za kizazi (*DNA*) za Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry zinaendelea kufanya kazi. **Aisha Maamiry** anasomea Sharia nchini Iran. Mwenye-ezi-Mngu amjaalie alikuze jina la Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry – Insha'Allah.
3. Waqf Commission of Kenya – kama tulivyo tangulia kueleza chanzo cha Kamati hii ya Waqf misingi yake imejengwa kwa utaaklamu wa sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry. Hadi hii leo, mmoja kati yaw a-Kamati wa nane ni lazima awe Chief Kadhi wa Kenya. Huu ni mmoja kati ya Urithi mkubwa.
4. Maamuzi ya kesi katika Mahkama Kadhi – Ndugu yangu Salim Maamiry amepokea kwa Sh. Muhammad bin Sheikh b. Muhammad Al Waaily kuwa yeye alikuwa akitumia nakili za Maamuzi ya kesi za Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry.
   — Sh. Muhammad b. Sheikh alizaliwa 1936. Akasoma Riyadha na Madrasatun Najah huko Lamu. Akasoma kwa Syd. Muhammad

Adnan Al-Ahdaly, Sh. Muhammad Ali Al-Maawy na kwa Syd. Ali Badawy.

— Sh. Muhammad b. Sheikh akawa Mwalimu Madrsatun Najah na pia akasomesha Garissa na Mafia.
— Alichaguliwa kuwa Kadhi wa Lamu 1960.
— Ustadh Harith aliwahi kumuuliza Shekhe wake, Sh. Muhammad Kassim Mazrui, "Ni nani kati ya Ma-Kadhi wake walokuwa bora?" Jawabu ya Sh. Muhammad Kassim ikawa:

i. Sh. Ali b. Muhammad Ali Al-Maawy alikuwa hodari sana kwa upande wa Fiqhi
ii. Sh. Muhammad Jawadi Abdul Wahab Jamalil Leyl (mzaliwa wa Ngazija 1916) alikuwa hodari sana kwa kuwashawishi watesi mume na mke wasiwachane, na waendelee maisha ya uke na ume kwa mapenzi na amani. Huyu amekulia Zanzibar na Lamu, akasomea Unguja kwa nduguye, Syd. Alawi, na kwa Syd Abdul Hasan Ahmad Jamalil Leyl. Lamu amesoma kwa Syd. Ahmad Badawy na kwa Syd. Muhammad Adnan. Amesomea TIBBA kwa Syd. Idarus b. Saleh. Alichaguliwa kuwa Kadhi 1957.

iii, Nae Sh. Muhammad b. Sheikh b. Muhammad Al-Waaily alikuwa hodari sana katika uamuzi wa kesi. Na kama tulivyo eleza hapo juu, yeye alitumia nakili za Maamuzi ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry kama kiegezo chake. Amenakiliwa kusema kuwa Maamuzi ya Kesi alizozinakili Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry zinatumika kama kiegezo (*reference*) katika Mahkama za Kadhi.

Kwa hivyo Urithi (*Legacy*) wa Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry unaendelea – *Alhamdu Lillah*!

Mausio Ya Wanavyuoni Kabla ya Kufa Kwao

- Sh. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui alikufa Mombasa – 12 Mfungo Tano 1312 A.H. (14 Agosti 1894). Wakati wa *sakaratil-mauti,* Sh. Ali b. Abdalla Naf'i alimkabidhi binamu wake, Sh. Suleiman b. Ali Khamis Mazrui ulezi wa mwanawe, Sh. Al-Amin, kwa maneno haya: **"Nakukabidhi mwanangu huyu leo duniani, unirudishie mwenyewe kesho Akhera!"** Jawabu ya Sh. Suleiman ikawa***: "Insha'Allah!"***

- Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikufa Mombasa – 26 Mfungo Tatu 1372 A.H. (9 January 1910). Sheikh aliusia kabla ya kufa kwake kuwa kaburi lake lisiwekewe alama yoyote – hii ndio maana halijukani hasa kaburi lake lilipo katika maziara ya Maamiry, Mgandini, Bondeni, Mombasa.

- Sh. Al-Amin b. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui alikufa Mombasa – 15 Mfungo Tano 1366 A.H. (1 Aprili 1947). Kabla ya kufa kwake aliwaita jamaa zake wa Ki-Mazrui (kwa upande wa baba) na Ki-Shatry (kwa upande wa mama) na kuwausia mambo matatu:

  — Madeni yake yalipwe kabla ya kufa kwake
  — Kwa kuwa ni Kadhi Mkuu wa Kenya, Serikali itataka kumfanyia Mazishi Rasmi. Kwa hivyo akawaomba jamaa wasimame kidete ili asifanyiwe Mazishi ya ki-Serikali.
  — Akaomba katika watakao beba jeneza, Wanafunzi wake wawepo mbele ya jeneza lake.

  Ama wakati wa kufa kwake, Sh. Al-Amin alikuwa amezingirwa na wakeze wote wawili, wanawe wa kike na kiume, na binamu wake, Sh. Muhammad Kassim Mazrui. Kabla ya sakarati alimmuliza mkewe, Bi. Swafia binti Suleiman, "Jee! Sasa ni saa ngapi?" Akajibiwa kuwa ni wakati wa Alasiri. Hapo akamuomba Bi. Swafia amtawadhishe, akaswali kwa kulala ikiwa amewekewa mito ya kumuinua. Baada ya kutoa salamu, ikaonekana midomo yake afunga na kufungua – akishahadia na kusallim amri. Hapo Malakul Maut akafanya kazi yake na kuichukua roho yake. Nae akaungana na Ammi yake, Shekhe wake,

Sh. Suleiman Mazrui pamoja na kuungana na babaake, Sh. Ali b. Abdalla katika *Barzakh*! – Alhamdu Lillah!

Katika jumla ya Urithi alotuachia ni:

- **Kuondoa** mila za kuweka Matanga.
- Swala ya Maiti ya kina mama ilianzishwa wakati wa kufa kwake.

Binti yake, Bi. Nafisa binti Al-Amin Mazrui alipewa jukumu la kuwatangazia kina mama kuwa Sh. Al-Amin amekataza asiwekewe Matanga. Vile vile akapewa jukumu la kuswalisha Swala ya Maiti.

- Sh. Muhammad Kassim Mazrui alikufa Mombasa – 5 April 1982. Usia wake aliuandika kwa njia ya Mashairi, na wakasomewa wanawake na binti yake, Bi. Maimuna Muhammad Kassim Mazrui.

  Sh. Muhammad alikuwa akiwaambia wanawe, "Nitakapo kufa, kitu kikubwa mutakacho kuwa hamutakipata kutoka kwangu, ni Dua ninazo waombea kila siku – Allah awape hidaya na awaongoze katika haki. Na kama ninavyo waombea, nami nitafurahi kama mutanikumbuka kwa Dua".

  Binti yake, Bi. Maimuna Muhammad Kassim Mazrui akapewa jukumu la kuswalisha Swala ya Maiti na kuwasomea kina mama Wasia wake kwa njia ya Mashairi.

Unaona Ushujaa wa kina mama na Malezi mema waloyapata kwa wazee wao:

- Bi. Nafisa Al-Amin Mazrui katika wakati mzito kama huo akaweza kusimama na kuwatangazia watu Wasia wa Sh. Al-Amin na kuwaongoza katika Swala ya Maiti – maiti mwenyewe akiwa ni babaake!
- Bi. Maimuna Muhammad Kassim Mazrui wakati wa masikitiko makubwa kama hayo, akaweza kusimama na kuwasomea kina mama Mashairi ya Wasia na kuswalisha Swala ya Maiti – maiti mwenyewe akiwa ni babaake!

Urithi Mwema! Kiigizo Chema!

Pongezi kubwa kwa:

- **Bi. Nafisa binti Al-Amin na kwa**
- **Bi. Maimuna binti Muhammad**

> Allah awalipe malipo mema ya Jannatul Firdaus kwa maongozi mema walotuachia – Amin.

***

Mpaka hapa nilipofika, namaliza kuhadithia "Maisha ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry (1850-1910)". *Ulamaa* huyu, kama nilivyotangulia kusema ni *Thaniya Thnaini - Swahaba (disciple)* wa Sh. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui (1825-1894). Kama alivyochangia Sh. Ali b. Abdalla kuzalisha *Ma-Ulamaa,* na yeye pia amewaendeleza wanafunzi wenzake na kuzalisha *Ulamaa* wengi wengine.

Sh. Ali b. Abdalla akamrithisha Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry darsa zake za Msikiti wa Basheikh. Nae Mwanafunzi-mwenza wa Sh Muhammad, Sh. Suleiman b. Ali Khamis Mazrui, akapokea na kumsomesha mwana wa Shekhe wake mpaka nae akawa *Ulamaa* kama alivyokuwa baba. Kwa hivyo Sh. Suleiman akarithishwa jukumu la ulezi wa mwana, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947).

Wakati wa *sakaratil-mauti* ya Sh. Ali b. Abdalla Naf'i, Sh. Suleiman b. Ali Khamis Mazrui alikabidhiwa ulezi wa mwana kwa maneno haya:

> **"Nakukabidhi mwanangu huyu leo duniani, unirudishie mwenyewe kesho Akhera!"**

Jawabu ya Sh. Suleiman ikawa***: "Insha'Allah!"***

Na kwa mausio hayo, jukumu zito likamwangukia Sh. Suleiman. *Alhamdu Lillah*! Akalitimiza jukumu lake kwa kumlea mwanawe huyu kwa mapenzi makubwa sana, akamsomesha upeo wa elimu yake na kumpeleka Unguja kwa Sayyid Ahmad b. Sumayt kwa masomo ya juu zaidi. Kisha akamuozesha Sh. Al-Amin binti yake, Bi. Swafia binti Suleiman.

Urathi wa Sh. Ali b. Abdalla ukaendelezwa kama ifuatavyo:

- Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akapokea elimu na kurithi Darsa

- Sh. Suleiman b. Ali Khamis Mazrui akapokea elimu kwa wote wawili na kurithi ule *Msahafu wa Tafsiri ya Jalaleni* yenya nukuu za Sh. Abdalla b. Naf'i na Sh. Ali b. Abdalla.
- Sh. Suleiman pia akapokea jukumu la kumlea Sh. Al'Amin na kumsomesha. Nae katika kusomesha kwake akatia nukuu zake katika aliyoirithi.
- Sh. Al'Amin akarithishwa elimu za Sh. Ali b. Abdalla Naf'i na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry pamoja na *Tafsiri ya Jalaleni*. Nae vile vile katika kusomesha kwake akatia nukuu zake.

Miongoni mwa wanafunzi wengi wa Sh. Al-Amin, ningependa kuwachagua wanafunzi watatu wafuatao na kueleza maisha yao kwa ufupi katika kitabu hiki:

1. Maalim Muhammad Abdalla Ghazali
2. Sh. Muhammad Ahmad Bereky Al-Lamiy
3. Maalim Said b. Ahmad Al-Kumri

***

Maalim Muhammad Abdalla Ghazali (1905-1959)

Maalim Muhammad Abdalla Ghazali, jina maarufu – Maalim Ghazali alizaliwa mwaka 1905 na kufariki 1959. Maalim Ghazali ajulikana sana kwa kuanzisha Madrasatul Ghazali kwa kufuata ushauri wa Mwalimu wake, Sh. AlAmin Mazrui. Sifa na umuhimu mkubwa wa Madrasa hii ni kuwa ndio Madrasa ya kwanza ilofungua milango na kusomesha watoto wa kike na wakiume, wakati ambao ilikuwa ni haramu kuwasomesha watoto wa kike. Madrasa hii baada ya kuvuma sana, ilichukuliwa na Serikali ya Ukoloni na kukuzwa kuwa Arab Girls Primary School – ambayo sasa inaitwa Mbaraki Girls Primary School.

Kwa hivyo sifa kubwa za Maalim Ghazali ni Madrasatul Ghazali.

Waalimu Wa Maalim Ghazali

- Bw. Ahmad Muhammad Matano, akijulikana zaidi kwa jina la "Bwana Mzee“. Huyu pia alikuwa Mwalimu wa Sh. Muhammad Kassim Mazrui. Bwana Mzee ni babu yao Sh. Abdillahi Nassir, Ustadh Ahmad Nassir na Prof. Abdilatif Abdalla.
- Sh. Said b. Ahmed Al-Kilindini – aliwahi kuwa Kadhi wa Takaungu, Vanga na Moshi.
- Sh. Al-Aufi – babu yake Bw. Muhammad Naaman Musisi
- Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947) – Huyu ndiye aliye wapa naswaha wanafunzi wake na wao waanzishe Darsa/Madrasa zao.
    - Naswaha hiyo ndiyo iliyo mshajiisha Maalim Ghazali kuanzisha Madrasatul Ghazal na Darsa za mjadala katika Msikiti wa Basheikh.
    - Maalim Ghazali alipokwenda kusoma kwa Sh. Al-Amin alikuwa tayari ameshakua Msomi aloiva.

Kazi Za Maalim Ghazali

- Maalim Ghazali kama tulivyotangulia kusema, alifuata wasia wa Sh.Al-Amin na kuanzisha Madrasatul Ghazal.

- Madrasa hii ilivuma sana, ikavutia wanafunzi wa kiume na kike. Madrasa hii ndio ilokuwa chanzo cha Arab School (Serani Primary).
- Sh. Al-Amin kwa kuikuza Madrasatul Ghazal alimpeleka binti yake, Ma Nafisa, na kuwa mmoja kati ya walimu.
- Vile vile aliwaandikia mashairi ya kuwashajiisha wanafunzi wa kike hasa ikifahamika kuwa wakati huo watoto wa kike walikuwa hawapewi nafasi ya kusoma. Wazee wengi wakiamini kuwa ni haramu kuwasomesha watoto wa kike.
- Utenzi huo walokuwa wakiimba wakati wa kufungia darasa, wakati wa kutoka ukiitwa "Banati Zetu, Banati":

1. Naanda kwa Bismilahi Walhamdu Lilahi
   Swala Llahu alaihi Muhammadi wasallama

2. Mewajibisha Rasuli Mwana mke na mvuli
   Kutafuta kila hali Elimu pakuisoma

3. Kwa amali kuipinda Elimu hukuifunda
   Ya kuswibu walotenda Haikuswihi fahamu

4. Abu Huraira Qala Kuifunda masaala
   Hupita alfu swala Za suna zilizo njema

5. Banati zetu banati Ni wake ni ummahati
   Haitengei hayati Ila wao kuwa wema

6. Tujipinde kuwaeya Kwa elimu na tabiya
   Kazi za mikono pia Kuwafunda ni lazima

7. Vijana tuwatungeni Tangu wali matumboni
   Hata kuja duniani Kwa ya swiha kuyandani

8. Wajibu wetu wazazi Vijana wakimaizi
   Ni kuwafundisha kazi Na elimu wakasoma

9. Elimu ndio dafina Na kazi hukuza jina
Tusiwatupeni wana Wakawa kana bahima

10. Haya tuwafundeni Ya dunia na ya dini
Wana tusiwatupeni Ujinga wakaandama

11. Ni madhambi juu yetu Tuwatupapo wenetu
Ni ipi jawabu yetu Mbele ya Mola Karima

12. Banati zetu banati Ni wake ni ummahati
Haitengei hayati Ila wao kuwa wema

***

Sh. Muhammad Ahmad Bereky Al-Lamiy

Jina Maarufu akijulikana kama Sheikh Bereky. Sh. Bereky alizaliwa Lamu tarehe 1 Aprili 1910 (20 Mfungo Sita 1328 A.H.) na kufa Mombasa, tarehe 6 Januari 1986. Alianza kusoma kwao Lamu kwa Sh. Abdalla b. Muhammad b. Omar Al-Khatib, Sayyid Ahmad Badawy, Kadhi Sayyid Abdalla b. Ahmad, Kadhi Sh. AbdulMajid b. Zahran na Mashekhe wengine wa Lamu.

29 April 1934 alihamia Mombasa na kuendeleza masomo zaidi kwa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui katika Msikiti wa Mazrui.

Kazi za Sh. Bereki

- Sh. Bereki alitumwa na Shekhe wake, Sayyid Ahmad Badawy kama Mwalimu kisiwa cha Vanga. Baada ya muda, kwa matatizo alokumbana nayo huko, alimwandikia barua Shekhe wake akimueleza hali ya maisha yalivyo Vanga na ugumu wa kuendelea kusomesha huko. Jawabu ya Shekhe wake ikawa ni kumshauri ahamie Mombasa. Na akifika huko, ende akajiendeleze ki-masomo kwa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui. Nae alipoipata barua hakukawia, ila aliaga wenyeji wake na kwenda zake Mombasa moja kwa moja hadi kwa Sh. Al-Amin. Hii ndiyo daraja alokuwa nayo Sh. Al-Amin kwa Maulamaa wa Lamu. Walimtambua Sh. Al-Amin na kumuheshimu. Na kubwa zaidi ni kuwa walikuwa wakiwashauri wanafunzi wao wende wakaongeze ilmu kwa Sh. Al-Amin.

  Mwanafunzi mwengine aliyeshauriwa ni Sayyid Ahmad kwenda kusoma kwa Sh. Al-Amin ni mwanawe yeye mwenyewe, Sayyid Ali Badawy. Sayyid Ali Badawy akasoma *Mustwalaul Hadith* na *Ilmul Meeqat*. Mustwalaul Hadith ni somo la kuweza kuzitambua Hadithi na kuweza kuzichambua zipi zinazofaa kutumiwa na zipi zisizofaa. Vile vile ukaweza kuziweka Hadithi katika mafungu ya daraja zake.

  Nayo Ilmul Meeqaat ni funzo linalo husiana na *Mathematical Geography*. Ukaweza kujua ilimu ya nyakati na vipi mwenendo wa

jua na mwezi unavyo athiri wakati na hali ya hewa baharini na nchini, na vipi unaweza kutambua nyakati za swala na kuandama kwa mwezi.

Uhodari alokuwa nao Sayyid Ali Badawy ni kuwa baada ya kumaliza masomo yake juu ya Ilmul Meeqat, aliporudi kwao Lamu, aliyaandika mafunzo yote ya Ilmul Meeqat kwa njia ya Mashairi kwa kiarabu, kisha akampelekea Shekhe wake, Sh. Al-Amin. Kwa furaha kubwa aliyokuwa nayo juu ya hidaya hiyo ya Mwanafunzi wake, Sh. Al-Amin akawa anawapa wanafunzi wake wengine ili na wao wanakili na kupata ruwaza.

Alipokufa Sh. Al-Amin 1947, Sayyid Ali Badawy kwa kutambulika kuwa alikuwa *Alim* alishika Ukadhi Mkuu wa Kenya kwa muda wa mwaka mmoja kabla ya kujiuzulu. Moja katika sababu zinazo semekana zilizo mpelekea kujiuzulu ni kuwa alikuwa hajawahi kufanya kazi Serikalini. Wengi walomtangulia walianza kazi Serikalini kama Ma-Kadhi kabla ya kupanda daraja ya Kadhi Mkuu wa Kenya.

- Sh. Al-Amin alimpokea Sh. Bereki kwa vizuri sana na kumuajiri kuwa Imam wa Msikiti wa Mazrui, na huku akijiendeleza ki-masomo. Sh. Al-Amin akampa makazi na kuishi pamoja na mwanafunzi-mwenza, Sh. Muhammad Kassim Mazrui.
- Sh. Bereki aliweka Darsa zake katika Msikiti wa Mbaruku kwa miaka mingi. Darsa za Msikiti wa Mbaruku alirithishwa na Sheikhul Islam, Baadae akahamia Msikiti wa Azhar, Baghani wakati wa kujengwa upya Msikiti wa Mbaruku.
- Sh. Bereki alizalisha Wasomi wengi. Kati yao wakiwa:
    - Sh. Abdurahman Hatimy, Mkanyageni/Mombasa.
    - Sh. Nassor Nahdy aliyeshika Ukadhi kwanza wa Mombasa, kisha Nairobi na baadae kuwa Chief Kadhi wa Kenya 1995-2002.
    - Sh. Ali Nahdy, nduguye Sh. Nassor Nahdy. Alikuwa Imam wa Msikiti wa Shibu.
    - Sh. Ali Gunda Seneda

- Ustadh Khamis b. Ahmad Al-Kumry, nduguye Maalim Said. Huyu ndiye aliyekuwa Khatibu wa Msikiti wa Mswalani pamoja na kuweka darsa. Ametowa wanafunzi wengi, mmoja wao akiwa Ustadh Naaman, Imam wa Msikiti wa Mazrui.
- Sh. Ali Darani aliyekuwa Kadhi wa Nairobi.
- Sh. Ali Mwenzagu alokuwa Kadhi wa Mombasa kwa miaka mingi.
- Maalim Shee, Imam wa Masjid Noor, Bondeni.
- Mwinyi Karama, Tabibu maarufu, Bondeni/ Mombasa. Yeye ndiye anaeziendeleza darsa za Sh. Bereki mpaka leo.
- Maalim Twaha aliyeweka Madrasa zake Msikiti wa Mbaruku.
- Shariff Ahmad Badawy aliyekuwa Imamu wa Msikiti wa Mahuru.
- Maalim Twalib Swaleh Elyan aliye anzisha Madrasatul Abrar.

***

Maalim Said b. Ahmad Al-Kumri

Maalim Said ni mzaliwa wa Mombasa 14 Mfungo Saba 1333 Hijria, sawa na March 1915, na akafariki tarehe 3 March 1983. Maalim Said alikuwa mwanafunzi wa Sh. Al-Amin Mazrui. Namna alivyokuwa akipendwa mwanafunzi huyu, Sh. Al-Amin akamfanya ndiye mwenziwe katika safari zake hasa za Tanganyika. Maalim Said alianza kupewa majukumu ya U-Imamu na kuwa Khatibu na kuswalisha swala ya Ijumaa kutoka 25 September 1937. Katika jumla ya kazi alizojitolea nazo Maalim Said ni:

- Kwenda kuwatembelea na kuwapa waadhi Wafungwa ndani ya Jela kuanzia 20 October 1945.
- Maalim Said alianza kutoa waadhi katika Sauti ya Mvita kuanzia 24 March 1952. Alikuwa na kipindi chake maalum kikiitwa “Kulla Sual ina Jawab!”
- Maalim Said alikuwa Khatibu na Imamu wa Msikiti wa Mswalani. Aliweka darsa zake Msikiti wa Mswalani na Madrasa yake ikiwa Floringi.

- Maalim Said aliweka Muhadhara pale Mwembe Tayari, akaweza kusilimisha watu wengi. Ikamlazimu kuanzisha Madrasa ya wale walosilimu hapo karibu na Mwembe Tayari.
- Maalim Said aliandika kitabu kidogo alicho kiita, "Kwa Nini Sikuwa Mkristo".

Tulipo mzungumza Sheikh Al-Amin Mazrui 24 December 2012, tulihadithia safari ya Sh. Al-Amin ya kwenda Moshi, Tanganyika ili akawakabili Makadiani katika Ngome yao. Safari hii, Sh. Al-Amin alifuatana na Maalim Said akiwa ndiye msaidizi wake na kupewa mikoba ya namna ya kufanya Da'awa. Makadiani walipopata habari ya safari ya Sh. Al-Amin, wakaazimia kumuua! Watu wema hupata hifadhi ya Allah. Kwani walipokuwa Tanga kwa Sh. Ali b. Hemed Al-Buhry (1889-1957), Makadiani walimfuata. Bahati kubwa ni kuwa Sh. Al-Amin alipata njozi kuwa jamaa wanakuja na azma ya kumdhuru. Akamwamsha Maalim Said, "Said, Said, Said!" Alipoamka, akamtaka ende akamuamshe mwenyeji wao. Sh. Al-Buhry alipokuja, Sh. Al-Amin akamwambia tutafutie gari tuondoke kwa haraka!" Bwana yule akastaajabu sana na kuuliza, "Sheikh kumezidi nini hata ukawa unataka kuondoka usiku mkubwa huu?" Sh. Al-Amin akajibu kuwa ameoteshwa kuwa Makadiani wanakuja kumdhuru.

Bwana yule akatafuta gari na wageni wake wakaondoka. Na kweli baada ya muda Makadiani hao wakafika na kubisha nyumbani kwa Sh. Al-Buhry. Alipowafungulia mlango akawauliza wanalotaka wakati huo. Jawabu yao ikawa wanataka kumwona Sh. Al-Amin. Bwana yule kwa kujua kusudio lake akawakaribisha na kuwachelewesha kwa kila njia ili kumpa nafasi Sh. Al-Amin azidi kwenda mbali zaidi. Jamaa hawakuamini alipowaambia hayupo. Akawapa nafasi wajikinaisha wenyewe. Wakatahayari na kuondoka.

Maalim Said b. Ahmad Al-Kumry alikufa 15 March 1983. Alhamdu Lillah! Allah alimpa kipawa cha kuushughulikia Umma kwa njia mbali mbali – kwa Mihadhara, Darsa na Madarasa, na kuwafuata wafungwa na kuwausia. Allah akampa hidaya na kuweza kuwarudisha wengi katika Iman na kuwasilimisha wengi. Allah amlipe mema kwa juhudi zake juu ya Umma.

****

Mukhtasari juu ya Maisha ya: Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry, Sh. Muhammad Bereki Al-Lamiy, Maalim Said Al-Kumry na Maalim Abdalla Ghazali

	Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry	**Sh. Muhammad Ahmad Bereki Al-Lamiy**
Kuzaliwa	1850	1 April 1910
Tarehe ya Kufa	9 January 1910	6 January 1986
Mahali pa kuzaliwa	Rastaka, Mjuakale, Mombasa	Lamu
Mahali pa kufa Mahali pa kuzikwa	- Mjuakale, Mombasa. - Makaburi ya Maamiry, Mgandini, Bondeni, Mombasa	- Baghani, Mombasa. - Makaburi ya Sarigoi, Mombasa
Kusoma Kwao	Ameaanza kusoma kwa babaake Sh. Kassim Al-Maamiry na baadae kwa Sh. Ali b. Abdalla Naf'i	Amesoma kwa Sh. Abdalla Khatib, Syd Ahmad Badawy n.k. Baadae pia akasoma kwa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui
Kazi walizozifanya	- Aliziendeleza Darsa za Sh. Ali b. Abdalla Naf'i katika Msikiti wa Basheikh - Kadhi Mkubwa wa Mombasa	- Alisomesha Vanga - Imam wa Msikiti Mazrui - Aliziendeleza Darsa za Sheikhul Islam, Syd Abdulrahman Saggaf (Mwinyi Abudu) katika Msikiti wa Mbaruku
Baadhi ya Athari walizoacha	- Wanafunzi wengi Ma-Ulamaa, mmoja akawa Chief Kadhi wa Kenya. - Hukumu za Sharia zinazotumiwa kama kiegezo - Mikakati ilotumiwa kuanzisha Waqf Commission.	- Wanafunzi wengi kati yao wakawa Walimu, ma-Imamu, ma-Kadhi, na mmoja wao akawa Chief Kadhi wa Kenya

	Maalim Said b. Ahmad Al-Kumry	**Maalim Muhammad Abdalla Ghazaly**
Kuzaliwa	March 1915	1905
Tarehe ya Kufa	15 March 1983	1959
Mahali pa kuzaliwa	Mombasa	Mombasa
Mahali pa kufa Mahali pa kuzikwa	Mombasa	Mombasa
Kusoma Kwao	Amesoma kwa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui na kwa Sh. Abdalla Al-Husny	Amesoma kwa waalimu kadha kabla ya kwenda kusoma kwa Sh Al-Amin b. Ali Mazrui
Kazi walizozifanya	- Alikuwa Khatibu na Imam wa Msikiti wa Mswalani - Akitembelea Wafungwa katika gereza la Shimo La Tewa - Akifanya mihadha Mwembe Tayari, akasalimisha wengi - Aliwafungua Madrasa ya wale waliosilimu - Aliweka Madrasa yake Msikiti wa Mswalani	- Alianzisha Madrasatul Ghazal. Madrasa ya kwanza kuwa na masomo ya kidini nay a skuli. - Aliweka Darsa Msikiti wa Basheikh
Baadhi ya Athari walizoacha	- Alisilimisha watu wengi kwa mihadhara yake na kutembelea kwake wafungwa - Mafunzo ya Dini kwa njia ya Radio	- Aliwafungulia milango ya kusoma watoto wa kike kwa msukumo wa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui

Jee ni Mafunzo Gani Tunayoweza Kujifunza kutoka kwa Wazee Wetu Hawa

- Wazee ndio RUWAZA ya kwanza ya watoto wao - "Umleavyo mtoto ndivyo akuwavyo"
- Sh. Kassim Al-Maamiry alikuwa kiigizo chema cha mwanawe - Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alilelewa na mzee wake na kuanza masomo yake chini ya mzee wake.
- Wazee waweza kuwajenga au kuwabomoa watoto wao - Alhamdu Lillah! Sh. Kassim alimjenga mwanawe na la ajabu ni kuwa baba akarudi kuwa mwanafunzi wa mwanawe baada ya Sh. Muhammad Kassim kuwa Alim.
- Maalim Said alichukua jukumu la kuwafuata Wafungwa katika jitihada yake katika Da'wa. Hivi ndivyo alivyotuusia Mtume (S.A.W.) kuwa tuufikishe ujumbe wa Dini japo kwa Aya moja tu.
- Maalim Ghazali alichukua jukumu la kuwafungulia milango ya Masomo watoto wa Kike. Leo Alhamdu Lillah, Dada na Binti zetu ndio wenye kufanya makazi na kuwasitiri wazee wao. Sikitiko ni kuwa watoto wa Kiume wanarudi nyuma na kushindwa na dada zao.
- Sh. Bereki aliziimarisha Darsa za Misikitini kama walivyofanya Mashekhe wake na kuihuisha Misikiti ikawa "Centre of Excellence"

Picha

Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry hakupenda kupigwa picha ingawa tayari wakati huo Camera zilikuwepo. Mambo mawili aliyo yakataza asifanyiwe ni:

- Kupigwa picha
- Kaburi lake kuwekewa alama za aina yoyote

Hii ndio maana hakuna picha yake, wala halijulikani kaburi lake. Ndio, ni hakika kuwa amezikwa katika makaburi ya Maamiry - Mgandini, Bondeni, Mombasa. Lakini hakuna anaeweza kukuonyesha kaburi lake. Hivi ndivyo nilivyo pokea kutoka kwa familia yake.

Picha za Maalim Ghazali na Sh. Ali b. Abdalla Naf'i nimezipata kwa Maalim Saggaf. Na zile za Sh. Bereki na Maalim Said kutoka kwa nakala za Bw. Faraj Dumila katika Coastweek. Sh. Bereki alikuwa hapendi kupigwa picha. Ilopatikana hii moja na ile alopigwa wakati wa safari yake ya Hija ilipokuwa hapana budi kupigwa picha.

Sh. Ali b. Abdalla Naf'i (1825-1894) – Mwalimu ni Kiegezo cha Muhammad Kassim Al-Maamiry (1850-1910)

Sh. Muhammad Kassim Mazrui (1912-1982)

Sh. Abdalla Swaleh Farsy (1912-1982)

Sh. Muhammad Kassim **Mazrui (1912-1982)** ni mjukuu wa Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry (185-1910)**. Alipewa jina la babu yake huyu na Masha'Allah jina likasibu na kumfuata babu yake khatua kwa khatua – ki-elimu, ki-tabia na ucha-Mngu, Alhamdu Lillah! Nae Sh. Abdalla Swaleh Farsy ni Mwanafunzi wa Sh. Ahmad Muhammad Mlomry **(1873-1936)**. Sh. Mlomry alianza kama Mwanfunzi Mwenza wa Sh. Al-Maamiry, kisha akarudi kuwa Mwanafunzi wa Sh. Al-Maamiry pale alipokufa Shekhe wao, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i **(1825-1894)**. Sh. Muhammad Kassim **Mazrui** na Sh. Abdalla Swaleh Farsy walikuwa wanafunzi wa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui **(1891-1947)**, mwanawe Mwalimu wa Sh. Muhammad Kassim **Al-Maamiry**. Sh. Al-Amin alilelewa na kusomeshwa na Sh. Suleiman Ali Khamis Mazrui **(1867-1937)**, kwanza akiwa Mwanafunzi Mwenza na baadae kama Sh. Mlomri akawa Mwanafunzi wa Sh. Al-Maamiry.

Alipokufa Sh. Ali b. Abdalla Naf'i mwaka wa 1894, mwanawe, Sh. Al-Amin b. Ali b. Abdalla Naf'i Mazrui ana miaka **4.** Baadhi ya wanafunzi wake wakiwa:

- Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry akiwa na umri wa miaka **44**

- Sh. Suleiman Ali Khamis Mazrui akiwa na umri wa miaka **27**
- Sh. Ahmad Muhammad Mlomry akiwa na umri wa miaka **21**

Maalim Muhammad Abdalla Ghazali

Sh. Muhammad Ahmad Bereki

Maalim Said b. Ahmad

Ustadh Harith Swaleh

Sh. Alamin Muhsin Muhammad Kassim Al-Maamiry (Mjukuu)

Bw. Salim Ahmad Muhsin Muhammad Kassim Al-Maamiry (Kitukuu)

***

Mwisho

Namalizia kuhadithia Maisha ya **Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry** kwa kumuombea yeye, pamoja na *Ma-Ulamaa* wenzake, nikiwajumuisha wazee, ndugu, jamaa, marafiki na Waumini wote kwa ujumla kwa kuungana na Malaika wanao ibeba Arshi ya Mwenye-ezi-Mngu katika Dua yao:

ٱلَّذِينَ يَحْمِلُونَ ٱلْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُۥ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِۦ
وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَىْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا
فَٱغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا۟ وَٱتَّبَعُوا۟ سَبِيلَكَ وَقِهِمْ عَذَابَ ٱلْجَحِيمِ ﴿٧﴾

Surat Ghafir 40:7 *Wale wanao ibeba Arshi (ya Allah), pamoja na wale wanao izunguka, wanamsabihi na kumhimidi Mola wao na kumuamini –* ***wanawaombea*** *msamaha wale walioamini kwa kusema,* ***"Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa Rehema na Ujuzi. Basi (tunakuomba) uwasamehe walio tubu na kuifuata Njia Yako, na uwaepushe na adhabu ya Moto wa Jahannam."***

رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّٰتِ عَدْنٍ ٱلَّتِى وَعَدتَّهُمْ وَمَن صَلَحَ
مِنْ ءَابَآئِهِمْ وَأَزْوَٰجِهِمْ وَذُرِّيَّٰتِهِمْ ۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ
ٱلْحَكِيمُ ﴿٨﴾

40:8 "Ewe Mola wetu! Waingize katika Bustani za Milele ulizo waahidi. (Uwajaalie wao pamoja na) wale walofanya mema miogoni mwa wazee wao na wake zao pamoja na vizazi vyao. Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima." ***

Bibliografia

1. *Sh. Abdalla Saleh Farsy - **"Baadhi ya Wanavyuoni wa KiShafi wa Mashariki ya Afrika"** toleo la Juni 1972 – Ukurasa 11*
2. *Mzee Rashid Abdalla Mazrui – Mahojiano nyumbani kwake Takaungu - 13 & 14 Februari, 2014*
3. *Maalim Abdulrahman Saggaf – Mahojiano nyumbani kwake Kizingo - 6 Juni, 2014*
4. *Ustadh Harith Swaleh – Mahojiano nyumbani kwake Mjuakale - 5 Juni, 2014 na 15 Oktoba 2015*
5. *Bw. Salim Ahmad Muhsin **Muhammad Kassim Al-Maamiry** – Mahojiano ya kwanza – 4 August 2014, na mahojiano mengine kadha wakati mbali mbali.*
6. *Bw. Ali Abdulkadir Maamiry (Ali Kitete) – Mahojiano kwa simu - 10 Aug 2014 na 7 Nov 2015*
7. *Sh. Hammad Muhammad Kassim Mazrui – Mahojiano kwa baruapepe - Aug 2014 na Nov 2015*
8. *Bw. Gharib Muhammad Kassim Mazrui – Mahojiano kwa baruapepe Nov 2015*
9. *Bi. Layla Muhammad Kassim Mazrui – Mahojiano kwa baruapepe Nov 2015*
10. *Coastweek juu ya Sh. Bereki na Maalim Said.*
11. *Ghalib Yusuf Tamim Baalawy – **Sh. Ali bin Abdalla bin Naf'i Mazrui (1825-1894): The Pioneering Role Model of The East African Muslim Reformers.***
12. *Dr. Abdulkadir Hashim - Administration of Waqf Institutions in the Kenya Coast.*
13. *Prof Issa Shivji katika Taazia yake juu ya Prof Mazrui – OCT 2014*
14. *Farouk Yusuf Tamim Baalawy – Uthibitisho wa tarehe za baadhi ya Mashekhe.*
15. *Prof Hassan Mwakimako - Conflicts and Tensions in the Appointment of Chief Kadhi in Colonial Kenya 1898-1960s.*